

**MADA : JUMBE KATIKA VIBANDIKO VYA MATATU**

**NA**

**MBURU PETER NG'ANG'A**

**REG NO. C50/61619/2010**

University of NAIROBI Library



0479833 6

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Umahiri  
katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

**2011**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya umahiri katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi:  \_\_\_\_\_

Tarehe: 01/11/2011

MBURU PETER NG'ANG'A

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri tulioteuliwa na chuo.

Sahihi:  \_\_\_\_\_

Tarehe: 2nd Nov - 2011

PROF. M.H. ABDULAZIZ

(Msimamizi)

Sahihi:  \_\_\_\_\_

Tarehe: 2/11/2011

DKT. AYUB MUKHWANA

(Msimamizi)

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mwalimu wangu wa zamani katika shule ya sekondari Bi. Kisovi aliyenichochea kuendelea na somo la Kiswahili katika viwango vya juu.

Namtambarukia marehemu dadangu Mary Wanjiru ambaye wema wake nitaishi kuukumbuka daima. Vile vile, naitabarukia mke wangu mpendwa Serah Muthoni ambaye amekuwa mhimili mkubwa katika masomo yangu tangu shahada ya kwanza na watoto wetu wawili, Joyann Gathoni na Lydia Murugi ambao wakati mwingi nimewanyima mahitaji muhimu ili kuyashughulikia masomo yangu.

## IKISIRI

Tasnifu hii inahusu jumbe zinazopatikana katika magari ya usafiri wa umma yanayojulikana kama Matatu. Utafiti wetu umefanyiwa mjini Nyahururu ambao ni mji unaopatikana katika jimbo la Nyandarua, takribani kilomita mia moja themanini kaskazini mwa jiji kuu la Kenya, Nairobi.

Utafiti huu umegawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza, tumelenga kutanguliza mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti na nadharia tete zitakazotuongoza katika utafiti wetu.

Aidha tumeziangalia sababu zetu za kuchagua mada pamoja na upeo na mipaka ya uchunguzi wetu, yaliyoandikwa kuhusu mada yetu, msingi wa nadharia na hatimaye mbinu zilizotumika katika utafiti huu.

Sura ya pili imelenga kuchunguza mitindo iliyotumiwa katika maandishi ya vibandiko. Sura ya tatu imeshughulikia matumizi ya sentensi na tamathali za usemi pamwe na jumbe katika matatu.

Katika sura ya nne, tumechunguza hisia na maoni ya wasafiri na waandishi wa jumbe zenyewe kuhusu jumbe kwenye magari ya matatu.

Katika sura ya tano, tumetathmini matokeo ya uchunguzi wetu, na pia kutoa mahitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.



## SHUKRANI

Kazi hii imechukua juhudi za watu kadhaa ambao walichangia katika kufanikiwa kwayo.

Shukrani nazitoa kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siha njema wakati wote niliokuwa nikiwania kuimaliza kazi hii na kunisaidia kugharamia masomo yangu ya shahada ya umahiri.

Nawashukuru wasimamizi wangu Profesa Mohammed Abdulaziz na Daktari Ayub Mukhwana kwa ushauri wao si haba na kwa kunielekeza katika kipindi hiki chote cha kuifanya kazi hii.

Nawashukuruni kwa kuwajibika kwenu kila wakati nilipowahitaji. Mola awabariki na kuwaongoza katika yaliyo mema maishani mwenu. Nawashukuru wahadhiri katika Idara ya

Isimu na Lugha waliojitolea mhanga kuhakikisha kwamba kozi hii imefaulu. Wao ni pamoja na Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Mwenda Mbatiah, Dkt. Zaja, Dkt. Kineene, Prof. Wamitila, Prof. Habwe, Bw. Mungania na Dkt. Jefwa Mweri. Kwenu nyote hongera!

Sitawasahau watu wengine ambao kwa njia hii au ile walinipa msaada wao katika kipindi chote cha masomo yangu. Wao ni Dkt. Ndichu, Dkt. Mayaka na Dkt. Nabea wote wa Chuo Kikuu kishiriki cha Laikipia. Shukrani zingine ziwaendee wanafunzi wenzangu ambao tuliabiri chombo kimoja na 'kuvuka serengeti' kwa kuhimizana. Wao ni Margaret Too, Pamela Topesi, Mary Apopo, Mbula, Joyce Karinge na Joyce Mzane. Wengine ni Lincon Nyaga, Simon Mwanjala, Mwituu, Mwiraria, Amos Ngugi, Andrew Watuha, Kitali, Alex Kinyua, Muhanda, Oluga, Ngunjiri na Njuguna.

Mwisho ningependa kumshukuru Tabby kwa kuipiga taipu kazii hii na kuhakikisha imekamilika katika muda ufaao.

## YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU .....	iii
IKISIRI.....	iv
SHUKRANI.....	v
YALIYOMO.....	vi
SURA YA KWANZA.....	1
1.1 Utangulizi .....	1
1.2 Tatizo la Utafiti .....	1
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	2
1.4 Nadharia Tete.....	2
1.5 Sababu Za kuchagua Mada.....	2
1.6 Upeo na Mipaka.....	3
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	3
1.8 Nadharia.....	5
1.9 Mbinu za Utafiti.....	9
SURA YA PILI .....	11
MITINDO YA JUMBE KATIKA MAGARI YA MATATU MJINI NYAHURURU.....	11
2.1 Utangulizi .....	11
2.2 Dhana ya Mtindo .....	11
2.2.1 Grafiti kama Mtindo.....	13
2.2.2 Sheng kama Mtindo .....	15
2.2.2.1 Ufupishaji wa Maneno.....	17
2.2.2.2 Matumizi ya Mafumbo .....	17

2.2.2.3 Kubadilisha maana ya kimsingi ya neno kwa njia nyingine .....	18
2.2.3 Matumizi ya Sajili mbalimabali .....	20
2.2.3.1 Sajili ya Usafiri .....	21
2.2.3.2 Sajili ya Biashara .....	22
2.2.3.3 Sajili ya Dini.....	23
2.2.3.4 Sajili ya Magazeti .....	24
2.2.4 Ukiushi kama Mtindo .....	25
2.2.4.1 Ukiushi wa Kifonolojia .....	26
2.2.4.2 Ukiushi wa Kisintaksia.....	27
2.2.5 Hitimisho.....	27
SURA YA TATU .....	28
TAMATHALI ZA USEMI NA JUMBE KATIKA MATATU .....	28
3.1 Utangulizi .....	28
3.2 Methali.....	28
3.3 Sitiari.....	29
3.4 Tasfida .....	31
3.5 Chuku/Udamisi.....	33
3.6 Kinaya/Kejeli.....	34
3.7 Taswira.....	36
3.8 Matumizi ya Sentensi.....	37
3.8.1 Dhana ya Sentensi.....	37
3.8.2 Sentensi Sahili.....	38
3.8.3 Sentensi Ambatano .....	39

3.8.4 Sentensi Changamano.....	39
3.8.5 Hitimisho .....	41
SURA YA NNE.....	42
MAONI YA WASAFIRI KUHUSU JUMBE KATIKA MAGARI YA MATATU.....	42
4.1 Utangulizi. ....	42
4.2 Maoni ya Wanafunzi wa Kiume.....	42
4.3 Maoni ya Wanafunzi wa Kike.....	44
4.4 Maoni ya Wanaume. ....	45
4.5 Maoni ya Wanawake.....	48
4.6 Maoni ya Waandishi wa Jumbe. ....	49
4.7 Hitimisho. ....	50
SURA YA TANO.....	51
MUHUTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	51
5.1 Utangulizi. ....	51
5.2 Muhtasari wa Matokeo. ....	51
5.2.1 Maoni ya Wasafiri.....	53
5.2.2 Kuhusu Nadharia Tete. ....	54
5.2.3 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye. ....	54
MAREJELEO.....	56
Kiambatanisho (i).....	58
Kiambatanisho (ii).....	60
Kiambatanisho (iii).....	61



## SURA YA KWANZA.

### 1.1 Utangulizi.

Vibandiko vibebavyo jumbe za kila aina vinapatikana katika magari mengi ya usafiri wa umma kama vile mabasi, mabasi madogo na magari yanayotambulika kama matatu mbali na yale ya kibinafsi.

Kulingana na gazeti la Daily Nation (4-12-2010 uk. 5) kuna magari mengi ya matatu ambayo hutumiwa na kiasi kikubwa sana cha abiria wa kila umri na tabaka. Baadhi ya wasafiri ni wafanyikazi na wafanyabiashara ambao wanatumia usafiri huu kila uchao. Katika matatu hizi kuna vibandiko vibebavyo jumbe za kila aina. Jumbe hizi ni pamoja na jumbe kuhusu uchumi, siasa, ndoa, mapenzi, maadili, dini na hisia za watu binafsi. Ni jumbe za aina hizi tulizozishughulikia katika tasnifu hii.

### 1.2 Tatizo la utafiti

Kama tulivyotanguliza katika kazi hii, magari ya matatu hutumiwa na watu wengi wa kila umri na tabaka kila siku hapa nchini. Kutokana na uchunguzi wetu wa awali, jumbe nyingi katika magari ya matatu hulenga watu mbalimbali. Jumbe hizi huwa zinapitisha mawazo muhimu kwa wasafiri wanaoyatumia magari haya ya matatu. Japo jumbe hizi zinayo mafunzo mengi kwa jamii, si wengi wanaozitilia maanani. Vile vile hakuna utafiti unao tathmini mbinu zilizotumiwa katika jumbe hizi na maoni ya wasafiri wa magari ya matatu uliofanywa hapo mbeleni. Tatizo letu hapa lilikuwa kubainisha udhahiri wa jumbe hizi; kuchunguza mitindo iliyotumiwa ili kuwavutia wasomaji na hivyo kuzisoma jumbe hizi na kuzitafakari.

### **1.3 Madhumuni ya utafiti**

Kwanza, utafiti wetu ulidhamiria kuchunguza jumbe katika vibandiko vinavyopatikana kwenye magari ya matatu ili kutathmini udhahiri wake katika mawasiliano. Tumejaribu kubaina umuhimu wa jumbe hizi ambazo hazitiliwi maanani na watu wengi. Vile vile, tumelenga kuchunguza mitindo mbalimbali iliyotumiwa kuandika jumbe hizi na pia kubaini kama jumbe hizi zimelengwa hadhira fulani maalumu. Hatimaye, tumechunguza jinsi mitindo ya uwasilishaji imechangia katika kuufikisha ujumbe kwa hadhira.

### **1.4 Nadharia tete.**

- a) Jumbe katika magari ya matatu zinapuuzwa na wasafiri.
- b) Jumbe katika magari ya matatu zimelengewa hadhira anuai.
- c) Mitindo mbalimbali imetumiwa katika jumbe ili kuvutia hadhira lengwa.
- d) Wasafiri katika magari ya matatu wana maoni tofauti tofauti kuhusu jumbe katika magari haya ya usafiri wa umma.

### **1.5 Sababu za kuchagua mada.**

Usafiri wa magari ya matatu unatumiwa na abiria wengi sana na wa kila aina kila siku.

Katika gazeti la Daily Nation (4-12-10 uk 5), kumetajwa kuwa kunacho kiasi cha matatu 20,000 mjini Nairobi na kiasi cha matatu 60,000 kote nchini Kenya ambazo zinawasafirisha abiria kila siku. Hivyo, jumbe katika matatu hizi hufikia watu wengi ambao wanaweza kufaidi kutokana na kusoma na kuzitafakari jumbe hizi.

Katika utafiti huu, tumekusudia kuwadhihirishia wasafiri wa magari ya matatu kwamba kuna jumbe muhimu ambazo kwazo mambo muhimu yanayohusu maisha ya watu wa kila aina yanaangaziwa. Tumejaribu kuondoa kalautala zilizomo na zinazowafanya abiria wengi kutozingatia jumbe hizi na kuzipuuzwa na kuthibitisha kwamba jumbe hizi ni muhimu kama zile zinazopatikana katika vitabu, magazeti, majarida na nyenzo za habari zinginezo.

### **1.6 Upeo na mipaka.**

Katika utafiti huu, vibandiko ambavyo vimeshughulikiwa ni vile vinavyopatikana kwenye magari ya matatu peke yake na sio magari mengineyo. Hii ni kwa sababu magari ya matatu yanatumiwa na idadi kubwa sana ya watu wa matabaka na umri tofauti mjini Nyahururu.

Utafiti huu umejikita katika vibandiko vilivyoandikwa katika lugha ya Kiswahili na Sheng na sio katika lugha zinginezo. Hii ni kwa sababu Kiswahili na Sheng zimejibaini kama lugha maarufu kwa sekta hii ya usafiri hasa kwa utingo na madereva na vile vile ni lugha zinazotumiwa sana na vijana wengi mijini na mashambani.

Uchunguzi wetu umelenga magari ya matatu katika mji wa Nyahururu peke yake na ni vibandiko vilivyopachikwa ndani ya magari ya matatu vinavyolenga abiria na wala sio vile vya nje ya magari ambavyo vinalenga wapita njia Nyahururu ni mji wa kadiri na kwa hiyo utaweza kuwakilisha miji midogo na vile vile miji mikubwa.

### **1.7 Yalioandikwa kuhusu mada.**

Sio watafiti wengi ambao wamelishugulikia swala hili la jumbe katika magari ya matatu nchini Kenya. Hata hivyo, tafiti kadhaa zimefanywa kuhusu maandishi ya mtindo wa grafiti ambao unakaribiana sana na ule unaotumiwa kuandika jumbe katika magari ya matatu. Nwoye, O (1993) alitafiti maandishi yanayopatikana katika vyoo vya wanafunzi wa vyoo

vikuu nchini Nigeria. Utafiti wake ulihusu jumbe katika kuta za vyoo hivi na ambazo zinajikita katika maswala ya kijamii peke yake. Utafiti wake umetufaa kwa vile umeweza kuwa kiungo muhimu cha mtindo katika utafiti wetu.

Kinyatti, L.M (2003) katika utafiti wake “Language as a tool of abuse against women”, alichunguza maandishi yanayopatikana ndani na nje ya magari ya matatu jijini Nairobi, Kenya. Utafiti wake ulifanyiwa matatu zilizohudumu katika maeneo ya Buruburu, Lang’ata, Kibera na Dagoreti. Uchunguzi huu ulidhamiria kuangazia jumbe ambazo zilionyesha maoni ya wahudumu wa matatu kuhusu mwanamke na jumbe zilizotumiwa katika magari ya matatu kumdunisha na kumdhalilisha mwanamke. Kwa hivyo tofauti kubwa ya utafiti wake na wetu ni kwamba alitafiti jumbe zilizolenga hadhira fulani maalumu yaani; ya kike katika jamii pana. Nairobi ni jiji kubwa kinyume na Nyahururu kwa hiyo jumbe zinazopatikana katika matatu huenda zikatofautiana katika miji hii.

Innocent Chilwa (2007) katika uchunguzi wake wenye kichwa “Religious vehicle stickers in Nigeria”: *A discourse of Identity, Faith and Social Vision*, alichanganua namna vibandiko vya magari yote kwa jumla hujenga utambulisho wa kibinafsi na wa kimakundi. Chilwa, alifanya utafiti wake katika miji miwili ya Lagos na Ota nchini Nigeria na data yake ilihusu magari sabini na matatu (73). Alithibitisha vile vibandiko vya magari vilivyoonyesha imani za kidini za watu na za makundi mbalimbali nchini Nigeria. Tofauti na utafiti huu, uchunguzi wetu umefanyiwa katika mji mmoja tu wa Nyahururu nchini Kenya ambao ni mdogo zaidi ikilinganishwa na jiji kubwa kama Lagos. Data ya utafiti wetu imehusisha magari mia moja



ya matatu na jumla ya vibandiko sabini na sita katika magari ya matatu vimechunguzwa.

Onchiri, H.O (2010), alitafiti maandiko aina ya grafiti katika magari ya matatu katika magari yaliyopatikana katika vituo vya Polisi, sehemu za kuegesha magari na katika gereji. Mtafiti huyu alichunguza kama kulikuwa na dhamira ya kiisimu katika maandishi ya mtindo wa grafiti katika magari ya matatu. Alitumia nadharia ya Pragmatiki Leksia. Katika uchunguzi wake, Onchiri (2011), alijikita katika jiji kuu la Kenya Nairobi katika mitaa ya Eastlands ambapo hii ni tofauti na utafiti wetu. Hata hivyo, mahitimisho aliyoyapata Onchiri yametufaa kimaudhui na hata kimtindo. Uchunguzi wake ni muhimu katika kazi yetu kwa sababu tumefaidi kutokana na njia zake za kukusanyia data.

### **1.8 Nadharia.**

Katika utafiti huu, nadharia iliyotumiwa ni nadharia ya Pragmatiki. Wasomi tofauti wemeielezea nadharia hii kwa kutumia istilahi tofauti tofauti.

Tuki (1996), wanasema kuwa pragmatiki ni nadharia ya vitendo ambapo hivi ni kusema kwamba nadharia ya pragmatiki huonyesha vile lugha inavyotumiwa katika kutenda kazi katika muktadha maalum. Massamba (2004), anaelezea pragmatiki kama taaluma ya isimu inayojishughulisha na uchunguzi wa lugha katika mawasiliano. Lengo kuu la taaluma hii ni kuchunguza namna lugha inavyotumiwa na wasemaji wake katika mazingira halisi. Naye Levinson (1983:5), anaitazama pragmatiki kama somo linalochunguza matumizi ya lugha. Kwa hivyo, kwa kuunganisha mawazo haya tunaweza kusema kwamba pragmatiki ni taaluma inayochunguza vile lugha hutumiwa kutenda kazi kulingana na muktadha ili kufanikisha mawasiliano katika jamii.

Waasisi wengi wa taaluma hii walikuwa ni Wamarekani ambao walikuwa katika mwelekeo tawala wa Isimu ya Marekani. Hata hivyo, hatuwezi kuwapuuza wengine kama Firth ambaye alishikilia kuchambua maana kimuktadha na Halliday na nadharia yake ya lugha na jamii.

Leech (1983), anatanguliza kusema kwamba mwanzo wa mwaka 1960, Katz na washiriki wake (Katz na Fodor (1953), Katz na Postol (1964), Katz (1964), walianza kuchunguza vile maana ingeunganishwa katika msingi wa nadharia moja. Lakoff na wengine (1971), walihoji kwamba sintaksia haingetenganishwa kihalali kutokana na matumizi ya lugha. Hivyo basi somo la pragmatiki likaingia katika ramani ya lugha. Ni kutokana na jambo hili ambapo matumizi ya somo hili la pragmatiki yalipanuka na kushughulikia muundo, maana na muktadha.

Mchango wa kuichumuza nadharia hii haukutolewa na wanaisimu peke yao. Kuna wanafilosofia wa lugha ambao walikuwa wakiichunguza pragmatiki hapo kitambo kidogo. Kwa hakika ushawishi mkubwa katika pragmatiki umetokana na wanafilosofia hawa wakiwemo Austin (1962), Searle (1969) na Grice (1975).

Kwa kuweka pamoja fikira hizi zote, Yule (1996:3), ameelezea mielekeo minne ambayo pragmatiki inajishughulisha nayo.

Kwanza, pragmatiki ni somo lichunguzalo maana ya msemaji au mzungumzaji. Hivyo ni kusema kwamba pragmatiki hutalii maana kama inavyowasilishwa na mzungumzaji au mwandishi na kufasiriwa mpaka kwa msikilizaji au msomaji.

Pili, pragmatiki huchunguza maana kimuktadha, maanake ufasiri wa kile watu wanachokimaanisha katika muktadha mahususi na jinsi muktadha huathiri kile kinachosemwa.

Mwelekeo wa tatu huangazia vile ujumbe mwingi huwasilishwa kuliko ule uliosema. Aidha huangazia vile mengi ya yasiyosemwa hutambuliwa kama kiungo cha yaliyowasilishwa ambapo hivi ni kusema kwamba pragmatiki huchunguza maana isiyoonekana waziwazi.

Mwisho, pragmatiki hutalii ujielezaji kulingana na masafa. Masafa yaweza kuwa halisi, ya kijamii na kidhana ambayo yanamaanisha msemaji na msikilizaji wana tajriba inayowapatanisha.

Wasomaji wengi wanakubaliana kwamba kuna vidokezo vitumikavyo katika maongezi.

Grice (1975), alipendekeza kwamba kuna mseto unaonekana wa chukulizi zinazoelekeza jinsi ya kufanya maongezi. Vivyo hivyo, Yule (1996), anazungumzia kanuni ya ushirikiano (co-operative principle) katika mawasiliano. Anaeleza vidokezo kama hali ambayo maneno yasemwayo yana jumbe nyingi zaidi kuliko maana yenyewe.

Vidokezo, kimsingi ni mfano wa vile yaliyosemwa huwa na maana zaidi lakini ili vidokezo viweze kusafiriwa, kanuni ya ushirikiano lazima ichukuliwe kwamba inatumika. Kanuni hii ya ushirikiano inafafanuliwa katika kanuni zingine nne ambazo zimekuja kujulikana kama kanuni za Grice. Kanuni hizi ni pamoja na;

(a) Kanuni ya ubora.

Kanuni hii inasisitiza kutolewa kwa habari zenye ukweli. Hii ni kusema msemaji au mwandishi anatakiwa kutotoa habari ambazo anaamini ni za uongo na kwamba asiseme kile ambacho hana uhakika nacho.

(b) Kanuni ya Idadi.

Kanuni hii inanuia kuufanya ujumbe uwe wa kufahamisha kama inavyohitajika. Msemaji au mwandishi asifanye ujumbe wake kutoa habari zaidi ya inavyokusudiwa.

(c) Kanuni ya uhusika.

Hii ni kanuni inayomhitaji msemaji au mwandishi kutoa habari zinazohusika na linalozungumziwa tu. Yaani, asiseme habari zilizoko nje ya mada au muktadha unaozungumziwa.

(d) Kanuni ya namna.

Kanuni hii inakusudia ujumbe utolewao uwe wazi, bayana na dhahiri. Aidha, ujumbe huu usiwe umefichwa, ambao hauna maana zaidi ya moja, mfupi na uliopangwa vizuri na ambao hautumii maneno mengi, marefu na yanayochosha. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba kanuni hizi ni chukulizi tu zisizoandikwa na ambazo zinatumika katika maongezi. Inachukuliwa kwamba wazungumzaji au waandishi watatoa kiasi cha ujumbe kinachotakikana tu, watasema ya kweli, watatoa yale tu ambayo yanahusu linalokusudiwa na wanajieleza kwa njia iliyo wazi kadri wanavyoweza.

Ni chukulizi ya kimsingi kwamba washiriki katika maongezi wanazingatia kanuni hizi za mazungumzo. Ni muhimu vile vile kuelewa kwamba ni waongaji ambao huwasilisha



maana kupitia vidokezi na ni jukumu la wasikilizaji kutambua maana inayowasilishwa kupitia ufahamu wao, yaani 'inference' kwa kingereza. Nadharia hii imetufaa katika utafiti wetu na ndiyo iliyotumika kutuongoza kuchambua data kuhusu ujumbe na maana zake katika vibandiko kwenye matatu mjini Nyahururu.

### **1.9 Mbinu za utafiti.**

Sehemu kubwa ya utafiti huu imekuwa nyanjani. Mbinu zilizotumiwa nyanjani zilikuwa mbili. Kwanza, mtafiti alinakili jumbe kutoka magari ya matatu mjini Nyahururu. Kwa vile kuna magari mengi mjini Nyahururu, mtafiti ametumia idadi ya magari mia moja. Mji wa Nyahururu una vituo vinne vya magari ya matatu na mabasi (Taz;kiambatisho (i)).

Mtafiti amechunguza magari ishirini na matano katika kila kituo. Kwa kutumia barua ya kujitambulisha, mtafiti aliwaomba idhini wahudumu na madereva ili kuingia katika magari ya matatu. Kujitambulisha kwake kulikuwa ni muhimu kwa vile asingefanya hivyo, wahudumu hawa wangeweza kukataa kutoa usaidizi muhimu ambao mtafiti aliuhitaji.

Mbinu ya pili nyanjani ilikuwa kufanya mahojiano ya moja kwa moja . Mtafiti aliwahoji watafitiwa ishirini (22) ambao wanawakilisha vikundi mbalimbali. Idadi hii ingawa ni ndogo ilimwezesha mtafiti kuwashughulikia watu wachache kwa ukamilifu zaidi. Vile vile, mtafiti aliwahoji waandishi wenyewe wa jumbe hizi ili kujua maoni yao kuhusu jumbe walizoziandika.

Mtafiti aligawanya watafitiwa hawa katika vikundi vifuatavyo;

i) wanafunzi

5 – wa kike

5 – wa kiume

ii) Wazee

5- wanaume

5- wanawake

iii) Waandishi wenyewe – wawili

Aidha vitabu vinavyozungumzia nadharia iliyotumiwa katika uchunguzi huu vilisomwa ili kutuwezesha kuielewa vilivyo nadharia yetu. Tulizisoma tasnifu za watafiti wengine ambao wameandika kazi kuhusu mada yetu. Hii ilikuwa kwa maana ya kulinganisha na kulinganua maoni yetu na ya watafiti wengine. Hatua ya mwisho ya utafiti wetu ni kuchanganua data tuliyoikusanya. Hii imefanyika kwa kuchunguza jumbe zilizopatikana ili kubainisha mitindo iliyotumika katika jumbe hizi. Vile vile, tumetathmini maoni na hisia za watafitiwa tulioweza kupata maoni yao. Hatimaye tumechunguza kama matokeo ya utafiti wetu yana mashiko yo yote ikilinganishwa na nadharia tete tulizoziorodhesha. Kisha tumetoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## SURA YA PILI

### MITINDO YA JUMBE KATIKA MAGARI YA MATATU MJINI NYAHURURU.

#### 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunakusudia kuchanganua mbinu za kimtindo zilizotumiwa katika jumbe zilizopatikana nyanjani kuhusiana na vibandiko vya matatu mjini Nyahururu. Tutaileza dhana ya mtindo na vile vile kuchanganua mitindo mbalimbali katika jumbe hizi na kuonyesha vile mitindo hii inachangia upokezi wa jumbe hizi kwa upande wa abiria na wa wahudumu wa magari haya.

#### 2.2 Dhana ya mtindo

Mbatiah, M (2000), **anaeleza** mtindo kama jinsi mtunzi wa kazi ya kisanaa anavyotumia lugha kujieleza. Anafafanua hoja hii kwa kusema kwamba uchanganuzi wa kazi ya kifasihi kimtindo unahusu mambo kama uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi zilizotumiwa, miundo ya sentensi, aya na beti n.k. Yaani mtindo hujumlisha vipengele vyote vya lugha.

Njogu, K. na Chimera R. (1999), wanasema kwamba mtindo ni tabia ya utungaji inayompambanua mtunzi mmoja na mwingine na wanaongeza kusema kwamba mtindo ni ufundi wa mwandishi fulani na ujuzi wake wa kujieleza.

Wamitila, K.W (2003), anasema kwamba mitindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuuwasilisha ujumbe wake. Kwake mtindo hueleza jinsi mwandishi anavyoiunda kazi yake. Dhana hii inarejelea sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha kwenye fani yake.

Mazoea haya ya mwandishi ni ya kuandika, kuteua msamiati, tamathali za usemi, taswira, uakifishi, sentensi na yanamtofausha mwandishi huyu na wenzake kiasi kwamba msomaji anaweza kusema hii ni kazi iliyoandikwa na fulani kwa kuisoma tu.

Tuanaweza kuunganisha maoni ya waandishi wote tuliowataja hapo juu na maoni ya Msokile M(1993)na (Senkoro, 1982:28), ambao wanasema kwamba mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hatimaye huonyesha nafsi na labda upekee wa mtunzi wa kazi hiyo. Hii ina maana kwamba sura atakayoipa msanii kazi yake itakuwa tofauti na nyingine iliyoandikwa na mtu mwingine. Hivyo, mtindo ni namna au jinsi mtunzi wa fasihi anavyoamua kuiwasilisha kazi yake kwa hadhira kwa njia ambayo itaipitisha dhamira yake.

Sehemu inayofuatia itaishughilikia mitindo michache tu ambayo hutumiwa na mtunzi kuwasilisha jumbe kwa msomaji. Mitindo itakayojadiliwa ni pamoja na grafiti, Sheng, sajili na ukiushi. Hii ni kwa sababu vibandiko vingi tulivyoviona kimbele katika magari ya matatu mjini Nyahururu vinaelekea kujikita kwenye mitindo hii.



### 2.2.1 Grafiti kama mtindo.

Kulingana na Jeanire (2006), asili ya mtindo huu wa uandishi ni neno la Kiitaliano “graffiato”. Haya ni maandishi yaliyoandikwa kwa kukwaruzwa sakafuni na kwenye kuta kwa kutumia vifaa vyenye ncha. Mtindo huu ulikuwa maarufu katika mji wa Ugiriki wa Ephesus. Rangi na mashine maalumu zilitumiwa kukwaruzia ambapo ilikuwa vigumu kuyaondoa hayo maandishi bila kutumia kemikali maalum.

Hapo awali maandishi haya yalipatikana kwenye kuta za nyumba, minara, mapangoni, majabalini na kwenye sakafu za saruji zisizokauka. Mwanzo mwanzo, grafiti ilichukuliwa na kutumiwa na watu ambao walikuwa wakizipinga tawala katika nchi za Magharibi na hivyo watunzi hawakujitokeza waziwazi. Aidha, grafiti ilitumiwa na vikundi vya kisiasa na watu binafsi kueneza mawazo yao. Walijitetea kwa kusema kwamba tabaka tawala lilikuwa likidhibiti nyenzo zote za kueneza habari kama vile redio, televisheni na magazeti. Vile vile walihoji kwamba hawakuwa na pesa za kufadhili nafasi katika magazeti kueneza maoni badalia. Baadaye grafiti ilitumika kama chombo cha kufanyia biashara. Kampuni maarufu ya mitambo ya tarakilishi, IBM, mnamo mwaka wa 2001 ilitumia mtindo huu wa grafiti kutangaza bidhaa zake katika miji ya New York, Chicago, Atlanta, Philadelphia, Los Angeles na Miami.

Hatimaye mbinu hii ilikubalika kama njia ya mawasiliano na ya kujielezea kwa watu ambao walikuwa wamegawanyika kijamii, kikabila na kimbari. Grafiti ilitumika pia kama njia iliyofaa kuwaleta watu pamoja kwa mawasiliano.

Kulingana na utafiti uliofanywa na Nwoye, O (1993), grafiti imetumiwa na wanafunzi wa vyuo vikuu katika kuta za vyoo ili kupitisha jumbe zao. Hivi sasa katika magari ya matatu hapa nchini Kenya, vibandiko vibebavyo jumbe za kila aina hupatikana katika magari haya. Vibandiko hivi vinajitokeza kama aina ya grafiti iliyopevuka.

Katika jumbe tunazozishughulikia, maandishi haya yaliandikwa kwa rangi tofautitofauti. Vibandiko vilivyopatikana ni vya rangi ya kijani kibichi na vilevile rangi nyekundu. Rangi hizi mbili zilitumiwa kuandika vibandiko hivi ili kuwavutia wasomaji na kuweza kuzisoma jumbe hizi.

Baadhi ya jumbe zilikuwa na mseto wa rangi za kijani kibichi na rangi nyekundu. Aidha, maneno fulani yaliandikwa kwa kutumia rangi ya kijani na katika neno au sehemu ya ujumbe unaotiliwa mkazo, rangi nyekundu imetumiwa. Hii kwa maoni yangu ina madhumuni ya kuichumuza sehemu ambayo wasomaji wanatakiwa kutilia mkazo zaidi na mfano wa ujumbe kama huu umetolewa hapa:-

“Juzi ilikuwa sare, jana vile vile. Sasa leo lipa *cash*.”

Katika ujumbe huu, neno ‘cash’ ambalo ndilo linaisitatizwa limeandikwa kwa rangi nyekundu ilhali yale mengine yote yameandikwa kwa rangi ya kijani. Kuna ushahidi wa maandishi mengine ya grafiti kama ilivyo katika mfano ufuatao;

“Gjue hali yako ya HIV”. Kupitia uchunguzi huu, mtindo wa grafiti umetumiwa sana kwa sababu unavutia wasomaji kwa vile umeandikwa kwa hati ambazo hazitumiwi katika maandishi ya kawaida.

### 2.2.2 Sheng kama mtindo

Sheng ni mfano wa lugha vipindi (msimu). Mtalam wa mambo ya lugha Busmah, H\_(1996), anaitazama lugha vipindi kama lugha iliyobuniwa na kikundi cha watu katika jamii. Lugha hii aghalabu huwa imejaa mafumbo na hubadilika kila kuchao.

Mifano ya aina za lugha vipindi ni misimu ya wanafunzi, misimu ya wawindaji, misimu ya wasomi na mingineyo. Asili ya lugha vipindi ni nchini Ufaransa. Ilichukuliwa kuwa lugha chafu kwa kusudi la kuficha mambo yasiyotakiwa kufanywa hadharani kwa mfano mapenzi, wizi na uuzaji wa mihadarati.

Wanaoitumia lugha msimu wanakusudia kuficha mambo kuhusu mbeko na miiko kwa kutumia ujanja wa matumizi ya lugha. Msamiati unaotumiwa katika lugha msimu ni msamiati maalum na usio rasmi na unayaeleza mambo katika njia isiyo ya kawaida. Lugha hizi za vipindi hazijali sheria za kisarufi na msamiati hudhamiriwa kufasiriwa kwa urahisi na wanaozielewa. Hapo mwanzo, lugha hii ya Sheng ilikuwa inatumiwa na watu wa tabaka la chini ingawa hali hii imebadilika kidogo hivi kwamba sasa inatumiwa pia na watu wa matabaka mengine Kenya.

Hapa nchini Kenya Sheng ina chazo chake katika jiji kuu Nairobi katika mitaa ya Eastlands mnamo miaka ya 1970 (rejelea Osinde, K.. 1986). Sheng ni neno linaloundwa kutokana na maneno mawili yaani Kiswahili na English. Hata hivyo lugha nyingine kama vile Kikikuyu, Kiluo na Kikamba hutumika, ingawa sintaksia inayotumiwa ni ya Kiswahili.

Sheng sasa inatumiwa na madereva na wahudumu wa magari ya matatu, katika magazeti, vyombo vingine vya habari na muziki hali ambayo imeifanya kuenea sana mpaka sehemu za mashambani. Msamiati wa Sheng hata hivyo ni tofauti kutoka sehemu moja ya nchi hadi

nyingine na vilevile sehemu mbalimabli katika miji. Sheng inayotumiwa katika mitaa ya vibanda kama vile, Dandora, Kibera, Mathare na Umoja jijini Nairobi itakuwa ni tofauti na Sheng inayozungumzwa katika miji mingine nje ya jiji kuu kama vile mji wa Nyahururu.

Katika utafiti wetu, matumizi ya Sheng yalijidhihirisha katika jumbe nyingi tulizozipata. Ushahidi uliopo ni kwamba Kiswahili na kiingereza zilitumika sana katika jumbe nyingi kama itakavyobainishwa baadaye katika mifano iliyotolewa.

Hata hivyo kuna matumizi ya lugha ya Kikikuyu ambayo ndiyo inatumiwa na watu wengi katika mji wa Nyahururu ambalo ndilo eneo letu la uchunguzi.

Tutatoa mifano michache ya matumizi ya Kiswahili na kiingereza;

- a) “ Usimharakishe driver, wewe ndiwe umechelewa”.
- b) “ Usiteme mate hapa, si una handbag?”
- c) “ Kupanda ni popote kushuka ni stage”.
- d) “ Conductor ni wa maana sana hutubebebea watu bila ukabila”.

Katika mifano hii minne, maneno yaliyopigwa mstari chini yake ni maneno ya kingereza lakini mengine yote ni ya Kiswahili. Mfano ufuatao ni mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kikikuyu, lugha inayotumiwa na watu wengi katika mji huu wa Nyahururu.

- e) “Wacha ugicagi”.

Neno “gicagi” ni neno la Kikikuyu linalomaanisha mashambani. Limeambishwa kwa kiambishi ‘u’ ambacho si kiambishi cha lugha ya Kikikuyu. Neno ‘gicagi’ maanake ni



Vijijini. Mtu anapoambiwa hivi anasutwa dhidi ya kuwa na fikira za vijijini ambapo, waishio vijijini wanachukuliwa kuwa nyuma katika mambo mengi ya kijamii.

Mbinu mbalimbali hutumika kuundia msamiati wa Sheng. Mifano ya mbinu hizi ni kama ifuatayo:-

### 2.2.2.1 Ufupishaji wa maneno

Mbinu hii inahusu udondoshaji wa silabi au sehemu ya neno na hivyo kufupisha neno hilo husika.

- Mifano
- i) Dereva - dere
  - ii) Buruburu - Buru
  - iii) Mheshimiwa - Mhesh
  - iv) Matatu - Mat

Mtafiti alipata mifano ifuatayo ya ufupishaji katika msamiati wa Sheng mjini Nyahururu;

- Mfano:-
- i) Dere yuko poa.
  - ii) Ukiingia kwa mat, usitoe viatu lakini toa fare.

Katika mfano (i) na (ii) maneno *dereva* na *matatu* yamefupishwa na kuandikwa kama *dere* na *mat* mtawalia.

### 2.2.2.2 Matumizi ya mafumbo

Fumbo ni mbinu ya matumizi ya maneno ambayo hayatolei maana waziwazi. Maana ya usemi au neno hufichwa ili yasijulikane kwa urahisi. (Kamusi ya Kiswahili Sanifu, 2004) Kwa mfano; “Kutupa mbao” katika lugha ya Sheng maana yake ni kuwa mwendawazimu au kukosa mwelekeo.

Katika uchunguzi wetu kuhusu jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu, matumizi ya mafumbo yalipatikana katika jumbe chache. Mifano ya jumbe zilizo na matumizi ya mafumbo imetolewa hapa;

- i) “Usinione nimetupa mbao, haja ndizo nyingi”. Katika ujumbe huu, maneno ‘nimetupa mbao’ yana maana kuwa mwenda wazimu au kukosa mwelekeo. Maana iliyofichwa ya ujumbe huu ni kwamba tusimwone kama mwenda wazimu anayezungumziwa kutokana na mambo anayoyafanya kwa kuwa mahitaji ndiyo yanamsibu kwa wingi.
- ii) “Yule manzi ametuvalia chupa leo”. Katika ujumbe huu ‘manzi’ maanake ni msichana na ‘ametuvalia chupa’ maanake ni kuvaa vazi linalombana sana.
- iii) “Anayemkamua ng’ombe wa jirani, arambe moto”. Ujumbe huu ambao ulipatikana katika matatu moja mjini Nyahururu umetumia maneno ‘anayekamua ng’ombe wa jirani’ kumaanisha anayefanya mapenzi na mke wa jirani. Hivyo mtu kama huyu anahukumiwa na mwandishi wa ujumbe huu arambe moto maana yake kwamba aadhibiwe vikali.

Katika mifano ya jumbe iliyotolewa hapa, mawasiliano yanakuwa siyo ya moja kwa moja bali msomaji au msikilizaji anabidiika kulifumbua fumbo kwanza ili kuelewa maana ya ujumbe uliowasilishwa.

### 2.2.2.3 Kubadilisha maana ya kimsingi ya neno kwa njia nyingine

Mbinu hii inabadilisha maana inayojulikana au iliyozoeleka ya neno fulani na kuipa maana nyingine ambayo inaeleweka tu na watumizi wa lugha ya Sheng.

Mfano: Neno	maana ya kimsingi	maana iliyobadilishwa
Mbuyu	aina ya mti mkubwa	Baba, mfidhili
Buda	Kobogoyo	Baba, tajiri au mzee

Katika kudhihirisha matumizi ya mbinu hii, tumetoa mifano ya jumbe mbili ambazo zilipatikana katika magari ya usafiri mjini Nyahururu.

Mfano: i) “Unapepea na VCT hujaenda”.

ii) “Juzi ilikuwa sare, jana vile vile sasa leo lipa cash”.

Maneno “unapepea” na “sare” yametumiwa kwa maana nyingine mbali na ile yake ya kimsingi kama inavyoonyeshwa hapa chini.

Neno	Maana ya kimsingi	Maana nyingine
1. Pepea	pigwa na upepo au vumbika	kuringa
2. Sare	mavazi rasmi	bila kulipia.

Hapo awali tulikuwa tumedokeza ya kwamba lugha vipindi zilikuwa zinachukuliwa kama lugha chafu. Lugha hizi ikiwemo Sheng hutumiwa kupamba lugha. Hii inasadia kuipa ladha lugha kwa watumizi wake ili iwavutie wazungumzaji wengine. Pili, lugha hii hutumiwa na wanaoielewa kuhifadhi siri. Mambo ambayo hayalengwi hadhira fulani husemwa kwa kutumia mbinu tulizozitungumzia hapo awali za uundaji msamiati. Tatu, Sheng husaidia kuikuza lugha fulani hasa pale maneno yanapoishia kukubalika katika lugha hiyo. Nne, Sheng huburudisha, huchekeka na hufurahisha watumiaji wake mbali na kujenga umoja na ushikamano kwa watumiaji wake. Mwisho, Sheng husaidia kuleta adabu kwa kutumia tasfida. Aidha, uundaji wake wa maneno ni rahisi kwa kuwa mitindo sanifu ya uundaji wa maneno haifwatwi.

Katika kishemu kifuatacho, tunachunguza matumizi ya sajili kama yanavyojidhihirisha katika vibandiko vipatikanavyo kwenye magari ya usafiri wa umma mjini Nyahururu.

### 2.2.3 Matumizi ya Sajili mbalimabali

Mathooko P.M (2007), anadai kwamba sajili pia huitwa rejista. Anasema kwamba sajili inaweza kuelezwa kama ni mtindo wa lugha kutegemea muktadha wa kijamii. Mathooko anaendeleza hoja yake kwa kusema kuwa sajili inaweza kuelezwa kama matumizi ya lugha katika viwango maalumu, kwa mfano maongezi ya kawaida, sheria, biashara, ukulima na teknolojia.

King'ei K.G (1992), anasema kuwa rejista katika lugha imetumiwa kueleza matumizi ya lugha katika uwanja maalumu. Anatoa mifano ya nyanja hizi maalumu kuwa ni dini, sheria, magazeti, michezo na nyenginezo.

Kwa kujumlisha mawazo ya wasomi hawa wawili tunaweza kuieleza sajili kama mtindo wa uandishi au usemaji na wa kimatendo ambao unatumia lugha katika uwanja maalumu kutegemea muktadha.

Sajili vile vile ni dhana inayotumiwa kuelezea sifa za kilugha zinazofungamana na kudhibitiwa na muktadha maalumu. Lugha hiyo inaweza kuwa ya kimaandishi au kimaongezi. Lugha inayotumiwa katika muktadha fulani inazo sifa kadhaa zinazobainishwa na muktadha wake. Kwa hivyo uteuzi wake wa msamiati, sarufi, uakifishaji, kiimbo na sauti huathiriwa na matarajio fulani ya kimuktadha (Wamitila: 2003)

Katika uchunguzi wetu, tulipata matumizi ya sajili ya usafiri, sajili ya biashara, sajili ya dini na sajili ya gazetini. Katika jumbe hizi, ni neno moja tu au machache yaliyoonyesha kuwa sajili fulani ilitumika na wakati mwingine ni kauli nzima ambayo inasheheni matumizi ya sajili fulani.



### 2.2.3.1 Sajili ya usafiri

Sajili ya usafiri hutumika sana katika magari ya usafiri wa umma na vile vile yale ya kibinafsi. Jumbe katika sajili hii huwa na msamiati mwingi wa usafiri kama vile 'safiri salama', 'dereva amehitimu', 'usiwe na wasiwasi', 'chungu mzigo wako' na mwingine mwingi. Baadhi ya jumbe hizi huwahimiza madereva kuzingatia sheria za barabarani na vile vile kuwaliwaza wasafiri wasiwe na hofu katika safari zao.

Utafiti wa jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu ulipata msamiati mwingi wa sajili ya usafiri katika jumbe zilizopatikana. Tumechambua mifano michache ya jumbe hizi.

Mifano;

(i) 'Chungu mzigo wako'.

Ujumbe huu ni ujumbe katika sajili ya usafiri kwa kuwa maneno 'chungu mzigo' ni maneno yanayofumbata dhana ya usafiri

(ii) 'Kupanda ni popote kushuka ni stage'

Sajili ya usafiri katika ujumbe huu inadhihirishwa katika matumizi ya maneno 'kupanda', 'kushuka' na 'stage (kishukio cha magari) ambayo yanatumika katika usafiri hasa katika magari ya umma.

(iii) 'Tafadhali jifunge mshipi'

Ujumbe huu unamsihi msafiri atumie mshipi ambao ni kifaa cha matumizi katika magari wakati msafiri anapoabiri.

Kwa hakika, sajili hii ya usafiri ndiyo iliyotumika kwa wingi zaidi katika jumbe zilizoshughulikwa mjini Nyahururu.

### 2.2.3.2 Sajili ya biashara

Sajili hii hutumia lugha ya kuchangamsha na ya kutia chumvi. Madhumuni ya sajili hii ni kutumia lugha ya kumvutia na kumshawishi mnunuzi ili ainunue bidhaa au huduma inayochuuzwa. Lugha hii huwa imejaa porojo za kila aina na kutiliwa chuku kwingi. kwa mfano “Tumia Aspro mbili kwa magonjwa ishirini” Lugha katika sajili hii huwa nyepesi na isiyozingatia mitindo sanifu ya mpangilio wa maneno katika sentensi. Vilevile, msanii huweza kuchanganya ndimi na kutumia msamiati usio sanifu.

Kwa mfano, tangazo la bidhaa ya sabuni kwa jina Jamaa: ‘jamaa we tiga tu!’. Katika tangazo hili kuna matumizi ya lugha ya Kikikuyu yaani ‘tiga’ maana yake acha. Sajili hii pia huambatanisha muziki mwororo pamoja na picha nzuri nzuri ili kuvutia wanunuzi wa bidhaa na huduma.

Msamiati tosha wa kibiashara ulipatikana katika jumbe nyingi kwenye magari ya matatu mjini Nyahururu. Kwa maoni yangu, hili lilikuwa jambo la kimakusudi ili wasafiri waweze kuelewa ya kwamba kazi ya “matatu” ni kazi kama kazi nyingineyo ambayo inafaa kuheshimiwa. Vile vile, jumbe hizi zinakusudiwa kuwahimiza wasafiri kutilia maanani kazi wanazozifanya kila siku.

Ili kuthibitisha matumizi ya msamiati wa sajili ya biashara, tutatoa mifano mitano kutoka baadhi ya vibandiko:-

- (i) “Lipa nauli bila shida”.
- (ii) “Biashara yangu haitaki mchezo”.

- (iii) “Utamu wa kazi ni pesa”.
- (iv) “Mkopo ni adui wa biashara”.
- (v) “Mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe”.

Kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu, msamiati wa kibiashara ambao umetumika ni maneno kama vile; lipa, nauli, biashara, kazi, pesa, mkopo na mtaji. Huu ni msamiati ambao unatumika katika shughuli za kibiashara katika mji huu wa Nyahururu na katika miji mingine mikubwa, ya wastani na midogo nchini Kenya.

### 2.2.3.3 Sajili ya dini

King’ei (1992), anadokeza kwamba mtindo huu wa kidini huwa tofauti sana na matumizi ya lugha ya kawaida. Mara nyingi huwa ni vigumu kufahamika na watu wasioitumia lugha hii ya kidini na muktadha wake wa matumizi.

Hata ingawa kuna dini nyingi ulimwenguni, kuna mambo yanayojitokeza katika lugha ya vitabu vyote vitakatifu vikiwemo Bibilia na Kurani takatifu. Dhana za ibada, mungu, dhambi, msamaha, adhabu na kadhalika ni baadhi ya mambo ambayo yanapatikana kwa wingi katika maandishi ya sajili hii.

Kulingana na Mathooko (2007), kuna uwezekano wa matumizi ya lugha za kigeni. Kwa mfano Kilatini na Kiyunani zinatumiwa sana katika vitabu vya dini ya Kikristo. Lugha ya Kiarabu nayo inatumika sana katika maandishi ya vitabu vya dini ya Kiislamu.

Katika dini nyingi, matumizi ya maneno yanayotaja Mungu yanakiliwa kwa herufi kubwa ya mwanzo kwa mfano Lamb, Lord, Light, Ngome, Njia na uzima katika Kikristo na Mtume, Allah, Malaika, Gibrili n.k. katika dini ya Kislamu. Katika mji wa Nyahururu, ilibainika kwamba sajili iliyopatikana katika jumbe nyingi ni sajili ya dini moja tu; Kikristo. Hata ingawa kuna Waislamu wachache, dini ya Kislamu bado haijasambaa kiasi cha kuweza kutumika katika matumizi ya kila siku.

Kwa hivyo, mifano iliyotolewa imeonyesha matumizi katika dini moja tu. Maneno yanayotumiwa yanaashiria dini ya Ukristo. Baadhi ya maneno ya kidini katika jumbe zinazoshughulikiwa ni Neema, Bwana Yesu Kristo, Ombea, utabarikiwa, unapobarikiwa n.k.

Msamiati tuliourodhesha unapatikana katika jumbe zifuatazo:-

- i) “Neema ya Bwana Yesu Kristo, iwe pamoja nanyi”.
- ii) “Ombea adui yako aishi siku nyingi ili unapobarikiwa ashuhudie mwenyewe”.
- iii) “Mganga wangu ni Yesu, jaribu wako mashuhuri”.

#### **2.2.3.4 Sajili ya Magazeti**

Magazeti hunuia kutoa habari ili kuburudisha, kujulisha na kuelimisha. Maandishi na lugha ya magazetini hutofautiana na mitindo mingine ya maandishi.

Tukiyachunguza maandishi katika sajili hii, tutakubaliana na King’ei (1992), anaposema kwamba vichwa vya habari huwa ni vifupi na vya kuvutia ili kunasa akili na macho ya msomaji. Vichwa hivi hueleweka kwa urahisi. Vichwa vyenyewe hutatanisha ili kuleta shauku.



Katika uchunguzi wetu, kauli za aina hii zilipatikana katika jumbe zilizoshughulikiwa. Kwa mfano, ujumbe katika kibandiko kifuatacho ni mfupi, wa kutatanisha na unaleta shauku; “Kaa nao ujue tabia zao”. Msomaji atajiuliza hawa ni akina nani wanaorejelewa na hivyo kuleta shauku.

Kama anavyosema King’ei (1992), uakifishaji katika maandishi ya magazetini hufanywa kwa nadra sana. Jumbe nyingi zilizoshughulikiwa hazikuakifishwa kamwe. Vile vile ushahidi wa matumizi ya mseto wa herufi zenye uzito wa wino kulingana na umuhimu wa habari ulipatikana; kwa mfano ujumbe “Unapepea na VCT hujaenda”.

Katika ujumbe huu, sehemu iliyopigwa mstari chini yake imeandikwa kwa wino mzito kuonyesha umuhimu wake.

#### **2.2.4 Ukiushi kama mtindo**

Lugha yo yote ile ina sheria zake. Kiswahili sanifu pia kina sheria zake zinazohusu muundo na sarufi yake. Maingiliano yo yote yanayoiathiri lugha kimuundo, kisarufi na hata kimsamiati ambayo yanazivunja sheria za lugha hiyo ni ukiushi wa kimatumizi (Shake, 1991).

Kulingana na Mbatiah, M (2000), ukiushi ni uvunjaji kimakusudi wa kaida za matumizi ya lugha ili kubuni njia mpya za kujieleza. Hivi ni kusema kwamba msanii anaitumia mbinu hii ya kuzivunja sheria za matumizi ya lugha ili kupata malengo yake katika kazi ya kifasihi.

Hata hivyo, mtazamo wa Kazungu. E.Kadenge (1982), ni tafauti kidogo na mtazamo tulioutaja hapo awali. Ukiushi hapa unatazamwa kuwa ni mkengeuko, mchepuko au upotovu kutokana

na matarajio ya namna ya kufanya mambo. Katika elimu mitindo, ukiushi ni kuandika au kuzungumza tofauti na kanuni na kaida zilizowekwa.

Maoni ya Kazungu yanakubaliana na ya Hartman na Stork (1973), pale ambapo wanaielezea dhana hii ya ukiushi katika lugha kama istilahi inayojumuisha tamko lolote ambalo halifuati kanuni zinazokubalika za sarufi au miundo ya kisemantiki ya lugha.

Ni maoni yangu kwamba ukiushi unaoelezwa na Hartman na Stork na Kazungu kwa upande mmoja unaonyesha kuwa ukiushi waweza kuwa si wa kimakusudi au unaotokana na athari zingine kama vile mazingira ,tofauti na Mbatia (2000), anayesema kwamba ukiushi ni tendo la kimakusudi

Jambo ambalo ni muhimu kwetu ni kwamba ukiushi utokeapo kimakusudi au pasi makusudi ,unapatikana katika viwango vyote vya lugha. Ni muhimu kutaja kwamba ukiushi unapatikana katika kiwango cha kifonolojia, msamaiti, sarufi, sintaksia na semantiki.

#### **2.2.4.1 Ukiushi wa kifonolojia**

Katika utafiti wetu ukiushi katika kiwango cha kifonolojia ulipatikana. Ukiushi huu unahusu kuongeza konsonanti /n/ kabla ya /d/. Kwa mfano katika ujumbe huu:- “Lipa nauli bila shinda”.

Konsonanti /n/ imeongezwa kabla ya /d/ katika neno {shinda}. Huu ni ukiushi wa kifonolojia. Ukiushi katika ujumbe unaozungumziwa hapa hata hivyo unatokana na athari ya lugha ya Kikikuyu ambayo ina wazungumzaji wengi sana mjini Nyahururu.

#### 2.2.4.2 Ukiushi wa kisintaksia

Ukiushi wa kisintaksia umebainika katika matumizi ya prepozisheni ‘ni’ na ‘kwa’.

Jumbe zilizoshughulikiwa zilibainisha matumizi yasiyofaa ya prepozisheni zilizotajwa. Katika ujumbe huu kwa mfano; “Ukiwa kwa gari unajifanya mkali na ukifika kwa nyumba wewe ni bubu”, tunapata matumizi ya ‘kwa’ badala ya ‘ni’ katika maneno gari (ni) na nyumba (ni).

Ukiushi mwingine ulipatikana pale ambapo uakifishaji katika sentensi umetumika kinyume na kanuni zilizomo za uakifishaji. Kwa mfano katika ujumbe ufuatao; “Karao alipe gari !!!” Katika sentensi hii alama ya uakifishaji (!), imetumiwa zaidi ya mara moja katika sentensi moja kinyume na ilivyo kawaida.

Kwa maoni yangu, mwandishi alidhamiria kuonyesha uzito ulioko katika onyo kwenye ujumbe unoazungumziwa na hivyo kuamua kutumia alama za uakifishaji kwa namna hiyo ili kutilia mkazo ujumbe huu.

#### 2.2.5 Hitimisho.

Tumejadili mitindo iliyopatikana katika jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu huku tukionyesha kwa kutolea mifano jumbe zilizosheheni mitindo iliyozungumziwa. Kama tulivyosema hapo awali, mtindo katika sajili ya usafiri ndio ulishughulikiwa kwa upana zaidi katika jumbe zilizopatikana mjini Nyahururu. Hata hivyo, sajili zingine zimechangia katika jumbe zilizoshughulikiwa.

## SURA YA TATU

### TAMATHALI ZA USEMI NA JUMBE KATIKA MATATU

#### 3.1 Utangulizi

Sura hii itashughulikia matumizi ya tamathali za usemi pamoja na sentensi zilizojibainisha katika jumbe zilizoshughulikiwa mjini Nyahururu. Tamathali za usemi zitakazoshughulikiwa katika tasnifu hii ni pamoja na methali, sitiari, chuku, kinaya, taswira na sentensi za aina mbalimbali. Tumezichagua tamathali hizi pamoja na sentensi kwa sababu utafiti umeonyesha kusambaa kwavyo kimatumizi katika jumbe tulizozishughulikia na kwa hiyo, vitatusaidia kuchanganua data yetu.

#### 3.2 Methali

Wamitila K.W (2003), anaeleza methali kama msembo wa kimapokeo ambao una muundo fulani mahususi, unaokumbukika na unaokusudiwa kuelekeza, kuadibu, kusuta, kulaumu na kushauri. Mbatiah (2000), **anasema** kuwa methali ni kauli fupi iliyosheheni maana na ujumbe na inayochukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha ukweli na busara.

Mulokozi (1989:14), anasema kwamba methali ni semi fupi fupi ambazo hueleza kwa muhutasari fikira au mafunzo mazito yaliotokana na uzoefu wa kijamii. Mara nyingi maelezo hayo huelezwa kwa kutumia tamathali hasa sitiari na mafumbo.



Kwa kifupi, methali ni semi fupi fupi zenye maana nzito na huwa zimejaa hekima ndani yake. Methali wakati mwingine hutegemea tamathali kama vile tashbiha, sitiari, kejeli, chuku na taswira.

Kwa kuzingatia idadi ya jumbe tulizoweza kuzikusanya, tuligundua ya kwamba matumizi ya methali hayakusambaa sana katika vibandiko kwenye magari ya usafiri wa umma katika mji huu wa Nyahururu.

Hivyo, ni ujumbe mmoja tu uliopatikana kuwa na matumizi ya methali. Methali iliyotumiwa kama ilivyotajwa, imetegemea tamathali ya sitiari ili kuundwa. Ujumbe uliokuwa katika kibandiko umetolewa hapa chini. “Pilipili usiyoila yakuashia nini”?

Katika methali hii, neno pilipili limetumiwa kama sitiari kuonyesha kitu kinachozungumziwa kina sifa za pilipili bila kutaja sifa yenyewe.

Kwa vile matumizi ya methali katika jumbe zilizokusanywa hayakusambaa, uchunguzi wetu haukuweza kuainisha methali zilizopatikana kwa kutumia vigezo vya kuziainisha methali katika makundi mbalimbali.

### **3.3 Sitiari**

Msokile, M (1993), anaifafanua dhana ya sitiari kama tamathali ya usemi inayolinganisha au kuhusisha vitu vilivyo tofauti kitabia au kimaumbile. Anaongezea kwamba athari za tamathali hii hutegemea kuhamishwa kwa maana na hisi kutoka katika kitu kimoja na kwenda katika kitu kingine. Aidha, vitu ama viumbe viwili vilivyotofauti kitabia ama kimaumbile vinahusishwa

kwa misingi ya sifa fulani iliyopo katika vyote viwili ama zaidi bila ya kutaja dhahiri sifa yenyewe.

Mtazamo wa Msokile unaelekea kukubaliana na wa Mbatiah (2000), kwamba ulinganishi tunaouzungumzia hauwi wa moja kwa moja. Vile vile, ulinganishi huu hautambulishwi kwa viungio kama vile “mithili ya” au “kama.” Sitiari, hivyo basi, hukuza sifa za ulinganishi kwa kusema kitu fulani ni kingine (Wamitila 2003). Kulingana na Wamitila (2004), sitiari zinajitokeza katika aina kadhaa za uainishaji. Wamitila amezitaja aina hizi za sitiari kama sitiari fiche, sitiari fifi, sitiari mseto, sitiari kuu na sitiari hisi mseto.

Katika utafiti huu, tulipata matumizi ya sitiari kwenye jumbe kadhaa. Mfano wa kwanza ni sitiari katika ujumbe huu; Mkopo ni adui wa biashara.

“ Mkopo” umemithilishwa na “adui” kwa vile vitu hivi viwili vina sifa zinazofanana, hata ingawa sifa zenyewe hazijatajwa.

Matumizi ya sitiari vile vile yanaonekana tukiuchunguza ujumbe huu wa pili.

“Mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe; bila jasho hupati”.

Neno nguvu katika ujumbe huu limetumiwa kama sitiari kwa vile limelinganishwa na mtaji. Inaelekea kwamba nguvu na mtaji ni vitu viwili ambavyo vina sifa moja inayofanana hata ingawa sifa yenyewe hatukutajiwa.

Katika utafiti wetu, tuliweza kupata matumizi ya sitiari hisi mseto. Hii ni aina ya sitiari ambayo kitu kisicho na sifa inayolinganishwa na kingine hupewa sifa hiyo ili kuchochea hisi fulani. Hebu tutazame jumbe hizi mbili;

(i) “Utamu wa kazi ni pesa”.

Katika kauli hii, kazi imepewa sifa ya kitu ambacho kinaweza kuonjeka na kupatikana kuwa kitamu.

(ii) “Biashara yangu haitaki mchezo”.

Usemi huu unaitazama biashara kama kiumbe chenye uhai na hivyo, kinaweza kuwa na hisi za kutaka au kutotaka.

### 3.4 Tasfida

Watu wa kila jumuiya huwa na tabia ya kutaja mambo yanayofikiriwa hayafai kutajwa hadharani kwa kuyafunika kwa maneno tofauti. Mbinu hii huitwa tauria lakini matumizi yaliyosambaa sana ni isitahi tasfida. Waandishi tofauti wanaielezea tamathali hii kwa maneno tofauti.

Njogu, K na Chimerah, R (1999), wanasema kwamba tasfida ni adabu ya lugha. Haya ni matumizi ya lugha safi iliyochujwa ili maneno machafu au yanayokirihi yasitumike. Tukisema ya kwamba “mtu fulani ni mja mzito”, tumetumia tasfida badala ya kusema mtu huyo “ana mimba”.

Wamitila (2003:194), anachangia zaidi kwa kusema kwamba tasfida ni matumizi ya maneno ya kupunguza ukali au uzito fulani. Lugha nyingine hutumiwa badala ya ile inayoudhi au ya kimatusi.

Tasfida inalo jukumu la kufichia hali fulani ambayo inahisika kwamba itakuwa na athari fulani zisizokuwa nzuri kwa wasomaji au hadhira. Tasfida wakati mwingine hujificha katika semi kama vile nahau na methali (taz Wamitila 2004). Kwa mfano nahau kwamba “ Maria ana mkono mrefu” ni tasfida ya “Maria ni mwizi” na vile vile katika methali “Nyani huchekana ngoko au ghubale”.

Maneno yaliyopigiwa mstari chini yake ni tasfida ya neno “kundu” ambapo likitajwa hadharani huenda likawachukiza wasomaji au hadhira.

Mbinu hii inahusu matumizi ya maneno ya kupunguza ukali au uzito fulani. Jambo ambalo lafikiriwa halitakikani kutajwa hadharani au waziwazi kwa sababu za athari fulani, huundiwa maneno mengine ili kuficha au kupunguza athari zisizotakikana.

Wakati wa kuhakiki jumbe zilizokusanywa, mbinu ya tasfida ilikuwa imetumika katika baadhi ya jumbe hizi. Mifano iliyo hapa chini inathibitisha hali hii.

i) “ Ubaya wa marehemu hakutumia juala”.

Katika ujumbe huu neno juala ambalo limepigiwa mstari ni tasfida. Ni neno linalotumiwa badala ya lile lililozoeleka “kondomu”

Kwa maoni yetu neno ‘kondomu’ likitajwa tu waziwazi linaweza kuitatiza hadhira hasa litajwapo mahali ambapo hadhira inajumuisha wazee na vijana wa umri tofauti.

ii) “ Kunyemelea mke wa mwingine ni kama ng’ombe kujipeleka kichinjio”.

Neno ‘kumnyemelea’ ni neno linalotumiwa kutajia hali ya kujihusisha kimapenzi. Ili kuipa lugha adabu inayostahili, mambo kuhusu mapenzi hayatajwi kiholela hivyo kukawa haja ya



kubuni lugha ambayo inaashiria kitendo kile kile lakini kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

(Taz. Njogu, K. na Chimera, R., 1999).

Juhudi hii ya kutumia lugha ili kuepuka mambo fulani waziwazi inabainika katika mfano wetu wa tatu;

iii) “Unapepea na VCT hujaenda.”

Neno kupepea ni tasfida kwa vile limetumiwa badala ya neno kuringa .

### 3.5 Chuku/udamisi

Tamathali hii kulingana na Mbatiah (2000), inatumia lugha ya kutilia chumvi aghalabu kwa madhumni ya kusisitiza. Tamathali hii inatumika kwa kuikuza sifa fulani kupita kiasi. Jambo ambalo labda halina sifa kubwa hutiliwa chumvi ili uzito unaokusudiwa ujidhihirishe kwa uwazi zaidi.

Katika maelezo yake, Wamitila (2003), anasema kuwa ni katika chuku ambapo sifa fulani hukuzwa kupita kiasi. Kukuzwa huku kunaweza kuwa kwa ukubwa au udogo. Nia hasa ya kutumia chuku ni kulifanya jambo fulani lilitokeze au lionekane kwa udhahiri zaidi.

Sababu nyingine ya matumizi ya chuku ni kuikuza sifa fulani akilini mwa msomaji au hadhira ili kuonyesha uzito uliopo. Kwa mfano;

“ Alipopigwa, alilia machozi yaliyojaa sufuria nzima” au “Damu ilimtirika kama maji ya mfereji”.

Maneno “sufuria nzima” katika sentensi ya kwanza na “maji ya mfereji” katika sentensi ya pili, yametumiwa kuonyesha wingi wa machozi yaliyotiririka na damu iliyomwagika mtawalia na sio kiasi halisi kilichotajwa.

Katika utafiti wetu, jumbe chache zilizoshughulikiwa zilikuwa na ujumbe au mambo fulani yaliyotiliwa chumvi. Kwa mfano:-

(i) “Ukiwa kwa gari unajifanya mkali na ukifika kwa nyumba wewe ni bubu”.

‘Bubu’ kama tunavyojua ni mtu ambaye hasemi kamwe. Hivyo tukisema mtu fulani ni “bubu” na wakati huo huo yeye husema katika muktadha mwingine ni kutilia chumvi mno. Labda tungenesema kwamba katika muktadha fulani mtu huyu huongea sana lakini awapo katika muktadha mwingine, yeye hasemi sana lakini hawezi akaitwa ‘bubu’ kwa maana ile iliyozoeleka.

(ii) “Mkopo ni adui” wa biashara.

Katika kauli hii kusema kwamba “mkopo ni adui” ni kutumia chuku. Adui ni jambo au mtu yeyote anayedhuru na kuharibu (TUKI 2004). Mkopo unaweza kutumiwa vizuri na kufanya biashara iimarike kwa hivyo kwa maoni yetu, kulinganisha “mkopo” na “adui” ni kutumia chuku au udamisi.

### 3.6 Kinaya/kejeli

Huu ni usemi wenye maana inayoashiria kinyume cha kile kinachosemwa Mbatiah (2000). Hutumiwa kuangazia utata wa maisha kwa kubainisha pengo lililoko baina ya jinsi mambo yanavyoonekana na jinsi yalivyo katika hali halisi. Hutumiwa vile vile kuubeza ujinga na udhaifu wa mwanadamu.

Wamitila (2003), anaelekea kukubaliana na maoni ya Mbatiah (2000) kwa kusema kwamba katika kinaya au kejeli, usemi fulani unaotumiwa una maana ya kinyume, yaani maana ya juu siyo ile iliyokusudiwa. Matumizi ya kejeli huchekesha na kuonyesha kinyume kwa njia isiyokuwa wazi.

Kejeli pia ni kusema au kutaja kitu kinyume na matarajio (Njogu, K na Chimerah, R1999).

Usemi ni kinaya pale ambapo jambo limetokea kinyume na matarajio ya watu

Kwa mfano “bahili” akiwa “mfadhili”. Ni jambo lisilotarajiwa mtu ambaye ni bahili akawa mfadhili hali ambayo ni kinyume na matarajio ya kawaida.

Wamitila (2004), anaongeza kwa kuainisha kejeli katika makundi mbalimbali.

Katika tasnifu hii tumechunguza matumizi ya kejeli ya kiusemi katika jumbe tulizozishughulikia na kutathmini kufaulu kwake katika kuwasilisha jumbe hizi.

Kuna mifano maridhawa ya matumizi ya kejeli katika jumbe zilizokusanywa mjini

Nyahururu. Hata hivyo, mifano itakayotolewa ni michache tu ili kuthibitisha matumizi haya.

(i) “Ili nifanikiwe nahitaji marafiki, ili nifanikiwe zaidi nahitaji maadui”.

Katika usemi huu, kinaya ni kwamba msemaji anahoji kwamba maadui wangemsaidia kufanikiwa zaidi kuliko vile marafiki wangemsaidia. Katika hali ya kawaida marafiki ndio wawezao kumsaidia mtu bali sio maadui.

(ii) “Wivu wako ndiyo bahati yangu”.

Kauli hii yote ni kinaya kwa sababu matokeo ya wivu kwa mtu mwingine huwa ni balaaa. Lakini katika usemi huu, bahati imekuwa ndiyo matokeo ya wivu kutoka kwa mtu mwingine. Hii ni kejeli ambapo jambo limetokea kinyume na matarjio yetu.

(iii) “Kazi kwa vijana, pesa kwa wazee.”

Katika usemi huu, kinaya kinajitokeza pale ambapo mtu fulani anafanya kazi na malipo yanamwendea mtu mwingine ambaye labda hakutia bidii zozote. Jambo hili ni kunyume na hali halisi ya mambo yanavyopaswa kuwa.

### 3.7 Taswira

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004), inaielezea dhana ya taswira kuwa picha ya mambo au vitu vinavyomjia mtu akilini mwake.

Katika maelezo yake Wamitila (2004), taswira ni dhana inayotumiwa kueleza neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Anazidi kusema kuwa taswira zinaweza kuwa za kimaelezo, maelezo ambayo yanaunda picha fulani au za kiishara.

Mtaalamu huyu anafafanua zaidi kuwa taswira zinaweza kuwa za aina nyingi kwa mfano taswira za uoni, taswira za harufu, taswira za joto, taswira za mwendo na nyingine nyingi. Katika tasnifu hii, tumechunguza matumizi ya taswira katika jumbe tunazozishughulikia na kutathmini kufaulu au kutofaulu katika kupitisha jumbe zinazokusudiwa kwenye vibandiko vinavyofanyiwa uchunguzi.

Taswira za aina tofauti zimejitokeza katika jumbe chache zilizochunguzwa kwa mfano;

(i) “Pilipili usiyoila yakuashia nini”?

Hii ni taswira ya harufu ya mwonjo. Neno ‘yakwashia’ lililotumiwa katika kauli hii linamfanya msomaji auhisi mwasho wa pilipili mdomoni mwake.



(ii) “Safari ni ndefu lakini nikiwa wa Yesu nitashinda”.

Msomaji asomapo ujumbe huu anaunda picha ya mtu aliye katika safari ndefu.

Hapa tunapata matumizi ya taswira ya mwendo.

(iii) “Kumnyemelea mke wa mwingine ni kama ng’ombe kujipeleka kichinjio”

Katika usemi huu, msomaji anapata taswira ya ngo’ombe akijipeleka kichijioni. Hii ni taswira ya ngo’ombe ambaye hujipeleka hatarini na kwenye maangamizi kwa hiari.

### **3.8 Matumizi ya sentensi**

#### **3.8.1 Dhana ya sentensi**

Mdee, J.S (1986), anaeleza kwamba sentensi ni tamko lenye kueleza fikira au hisi kwa kutumia neno au maneno yenye umbo na kwa maana ambayo itawasilisha ujumbe uliokusudiwa.

Katika kufafanua zaidi sentensi, Obuchi, M.S na Mukhwana, A. (2010), wanamnukulu Crystal (1991) kwa kusema kwamba sentensi ni kipashio cha kujieleza kinachosheheni fikra kamili. Wanaisimu Obuchi na Mukhwana wanafafanua sentensi mbalimbali. Tumezitumia sentensi hizi kuchanganua jumbe zilizokusanywa mjini Nyahururu.


Sentensi zilizotumiwa ni pamoja na sentensi sahili, sentensi ambatano na sentensi changamano. Tumekusudia kutumia aina hizi za sentensi kwa vile utafiti wa jumbe zilizokusanywa umeonyesha kujikita katika matumizi ya aina hizi za sentensi. Sehemu ya mwisho imeonyesha dhima ya sentensi zilizotumiwa katika jumbe hizi na kuthibitisha vile sentensi hizi zinavyosheheni kauli mbalimbali kama vile kutoa amri, kuthibitisha, kushauri, kuonya, kushauri, kutoa kauli yakinishi na vile vile kauli kanushi.

### 3.8.2 Sentensi sahili


Hizi ni sentensi za msingi kabisa. Jambo linalojitokeza katika sentensi za aina hii ni kule kuwa na kiima kimoja tu na kiarifu kimoja. Vile vile, sentensi hizi hutoa habari chache katika kueleza wazo moja tu. Sentensi sahili ni kishazi kinachojihimili na kwa hivyo hakijumuiki na kingine. (Taz: Kimani Njogu na wengine 2006).

Mifano iliyotolewa imebainisha matumizi ya sentensi sahili katika jumbe zilizokusanywa.


(i) **“Biashara yangu haitaki mchezo.”**



(ii) **“Mwenye wivu ameze wembe”.**



(iii) **“Karao alipe gari!!!”.**



Katika sentensi hizi tatu muundo wake ni wa sentensi sahili ambao unasimamia wazo moja tu kila moja. Aidha sentensi hizi zina kiima na kiarifu kimoja.

### 3.8.3 Sentensi ambatano

Sentensi ambatano ni muungano wa sentensi mbili zenye uzito sawa kwa kutumia viunganishi kama vile ‘pamoja’ ‘kisha’ ‘halafu’ na ‘lakini’ miongoni mwa vingine. Utafiti wetu wa jumbe katika magari ya matatu uligundua matumizi ya sentensi ambatano na baadhi ya viunganishi vilivyo tajwa hapo juu na kuunganisha sentensi sahili katika jumbe zilizoshughulikiwa.

Tutatoa mifano ya jumbe nne miongoni mwa nyingine katika data yetu zilizo na matumizi ya sentensi ambatano na kuonyesha viunganishi vilivyotumika kuunga sentensi hizi.

- (i) “Heri kununua gari kuliko kuoja mke mkorofi”.
- (ii) “Lipa deni la mwenyewe na utabarikiwa”.
- (iii) “Safari ni ndefu lakini nikiwa na Yesu nitashinda”.
- (iv) “Kazi ni kazi bora mtu asukume maisha”.

Katika mifano hii minne iliyotolewa, viunganishi “kuliko”, ‘na’, “lakini” na “bora” vimetumika kuunganisha kauli mbili pamoja.

### 3.8.4 Sentensi changamano

Sentensi za aina hii huwa na vishazi viwili au zaidi; kishazi huru na kishazi tegemezi. Vishazi hivyo huunganishwa kwa kiunganishi kitegemezi na hivyo kuzua sentensi changamano.

Katika jumbe zilizoshughulikiwa, tulipata uchache wa sentensi changamano. Hata hivyo mifano miwili iliyotolewa imeonyesha matumizi ya aina hii ya sentensi ambazo zimeundwa kwa vishazi viwili; kishazi huru na kishazi tegemezi.

i) Usiniite mjinga kwa kuniona mpole.

ii) Msiegemeane kwa gari kama hamjuani.

Katika mfano (i) na (ii) vishazi huru ni Usiniite mjinga. Katika sentensi (i) na msiegemeane kwa gari katika sentensi (ii).

Vishazi tegemezi navyo ni;

Kwa kuniona mpole katika ujumbe (i), na kama hamujuani katika ujumbe (ii)

Kwa kutathmini dhima ya sentensi katika jumbe zilizokusanywa, yalibainika matumizi ya kauli mbalimbali katika jumbe hizi. Tulipata kauli zenye jumbe za kushauri, kuonya, kuamrisha, kuomba na vile vile kauli yakinishi na kanushi, kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo ya jumbe zilizofanyiwa utafiti.

Tumetoa mifano maridhawa kwa kila aina ya ujumbe uliotolewa;

i) Ridhika kwa kile umepata – Kushauri.

ii) Fanya fujo unione – Kuonya.

iii) Karao alipe gari!!! – Kuamrisha.

iv) Tafadhali jifunge mshipi – Kuomba.

v) Utamu wa kazi ni pesa – kauli yakinishi.

vi) Usiidharau kazi yangu, yako hainisaidii-kauli kanushi.



### 3.8.5 Hitimisho

Sehemu hii ya sura ya pili imeangazia tamathali za usemi pamoja na sentensi ambazo zilijibainisha katika baadhi ya jumbe tulizozishughulikia katika magari ya matatu mjini Nyahururu. Katika baadhi ya jumbe zilizoshughulikiwa tumepata matumizi ya zaidi ya tamathali moja katika ujumbe mmoja. Kwa mfano ujumbe uliweza kujitokeza kama methali na wakati huo ukajitokeza kama fumbo.

Vile vile, katika matumizi ya aina mbalimbali za sentensi, sentensi sahili ambazo hubeba wazo moja tu zilisambaa katika jumbe nyingi zilizotafitiwa kinyume na sentensi ambatano na sentensi changamano ambazo matumizi yake hayakusambaa sana. Aidha, jumbe zilizochunguzwa zimedhihirisha sentensi zinazosheheni kauli mbalimbali zikiwemo kauli yakinishi na kauli kanushi.

Katika sura ifuatayo, tasnifu hii imechanganua maoni ya wasafiri na ya waandishi wenyewe kuhusu jumbe zipatikanazo kwenye magari ya usafiri mjini Nyahururu. Wasafiri hawa na waandishi wa jumbe zenyewe ni wa umri mbalimbali na vile vile wa jinsia zote mbili.

## SURA YA NNE

### MAONI YA WASAFIRI KUHUSU JUMBE KATIKA MAGARI YA MATATU.

#### 4.1 Utangulizi.

Sehemu hii imenuia kutathmini maoni ya wasafiri kutoka matabaka na umri mbalimbali kuhusu jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu. Mtafiti aliwahoji wanafunzi wa shule za sekondari ambao ni wa kiume na pia wa kike. Maoni yao wanafunzi hawa yamejadiliwa kulingana na jinsia, yaani maoni ya wavulana yamejadiliwa kando na ya wasichana.

Mtafiti pia alifanya mahojiano na watu wengine ambao ni wafanyikazi na wanaofanya biashara mjini Nyahururu ambao wanayatumia magari ya matatu katika shughuli zao za kila siku.

Vile vile, maoni yao yamejadiliwa kulingana na jinsia, aina za kazi na umri.

#### 4.2 Maoni ya wanafunzi wa kiume.

Wanafunzi waliofanyiwa utafiti katika jinsia hii walikuwa na umri kati ya miaka kumi na mitano hadi ishirini (15-20). Walikuwa katika madarasa tofauti. Kutokana na majibu ya mahojiano na mtafiti, ilibainika kwamba wao walikuwa wakizisoma jumbe katika magari ya matatu ya mjini Nyahururu kila wakati wanapoyaabiri asubuhi na alasiri wanapoingia shuleni na kurudi nyumbani.

Kundi hili la watafitiwa lilishabikia jumbe zilizoandikwa kwa mtindo wa Sheng. Walipotakiwa kueleza ni kwa nini walizipenda jumbe zilizoandikwa kwa mtindo wa Sheng, walijibu ya kwamba lugha hii ya Sheng ilikuwa maarufu kwao na ilikuwa rahisi kueleweka. Walidai kwamba Sheng ilikuwa ni lugha yao ya matumizi na wanafunzi wenzao katika mazungumzo ya kila siku.

Wengine katika kundi hili walisema kwamba walifurahishwa na jumbe katika lugha za Kiswahili na Kingereza. Hii ni kwa sababu lugha za Kiswahili na kingereza ni lugha rasmi katika shule zao na hivyo, jumbe zilizoandikwa kupitia lugha hizi mbili zinaeleweka kwa wepesi zaidi kwao.

Watafitiwa walitakiwa kuelezea ni mada zipi za jumbe katika mataṭu ambazo zinawavutia zaidi. Katika kujibu, jumbe ambazo zinazungumzia maisha ya binadamu kwa ujumla zilikuwa na wasomaji wengi. Jumbe ambazo hazilengwi hadhira fulani maalumu zilikuwa na wasomaji wengi katika kundi hili la watafitiwa. Hata hivyo, jumbe ambazo zilizungumzia mada kama vile dini na mapenzi ziliwapendeza baadhi ya wanafunzi wa kiume waliofanyiwa utafiti ingawa idadi yao haikuwa kubwa (asilimia ishirini).

Mtafiti aliwataka watafitiwa kubaini kama jumbe wanazosisoma zilikuwa na umuhimu wote maishani mwao. Maoni yao yalikuwa kwamba jumbe hizi zilikuwa muhimu katika kuelimisha vijana kuhusu maadili kama vile kuwaheshimu wazee wao na kutojiingiza katika uraibu ambao unaweza kuvuruga elimu yao kama vile kufanya mapenzi kiholela, uvutaji wa sigara, matumizi ya dawa za kulevya na vileo vingine.

Watafitiwa wengine walidai kwamba jumbe hizi zinatoa ujumbe wa kukanya watu wa kila aina dhidi ya kujiingiza katika tabia au mienendo isiyokubalika katika jamii. Aidha jumbe zingine ziliwaonya watu kwa kueleza yatakayotokea iwapo wanajamii wangepuuza maonyo yaliyotolewa. Hii kulingana na watafitiwa hawa iliwasaidia kuchukua tahadhari za mapema kabla janga halijatokea.

Baadhi ya watafitiwa katika kundi hili walisema kwamba jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu huwachangamsha wanapozisoma. Wengine walidai kwamba jumbe hizi ziliwasaidia katika kupata maelekezo muhimu kuhusu maisha.

#### **4.3 Maoni ya wanafunzi wa kike.**

Wanafunzi waliofanyiwa utafiti katika kundi hili walikuwa kati ya umri wa miaka kumi na mitano hadi ishirini (15-20). Wote waliotafitiwa walizielewa lugha za Kingereza, Kiswahili na Kikikuyu. Ilibainika kwamba watafitiwa hawa kama ilivyobainika katika kundi lililotangulia, walizipenda jumbe zinazowasilishwa kwa mtindo wa Sheng. Kwa kutoa sababu, walidai kwamba Sheng ni lugha ambayo imesambaa sana kimatumizi na takribani wanafunzi wote katika shule za mjini Nyahururu wanaweza kuwasiliana kupitia Sheng bila tatizo lo lote.

Baadhi yao hata hivyo, walipenda kusoma jumbe katika lugha za Kiswahili na Kiingereza. Mtafiti alipotaka kujua ni kwa nini walizipenda jumbe katika lugha za Kiswahili na Kingereza, wengine (asilimia arobaini) walisema kwamba wangependa kujizoeshwa kuzungumza lugha hizi mbili kwa vile katiba mpya imezipatia lugha hizi mbili nafasi kubwa.



Kwa hivyo kwa maoni yao, kujikita katika jumbe zilizowasilishwa kwa Kiswahili na Kiingereza kunawafanya wajihisi wazalendo zaidi.

Katika kundi hili la watafitiwa, mada ambazo zilipendwa na wengi ni zile zinazowasilisha jumbe kuhusu dini. Wote waliofanyiwa utafiti waliungama kuwa ni waumini wa dini ya Kikristo na kwa hivyo ujumbe katika sajili ya dini ya Kikristo ulipendwa na wengi. Idadi ndogo ya watafitiwa (asilimia kumi na tano) ilisema kwamba ilifurahishwa na jumbe kuhusu maisha kwa jumla.

Watafitiwa walitoa maoni yaliyokaribiana kuhusu umuhimu wa jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu. Wengi walidai kwamba jumbe hizi zina jukumu la kuelimisha na kufahamisha wasafiri. Aidha wengine walisema jumbe hizi zinawachochea kuchukua hatua au msimamo fulani maishani baada ya kuzisoma. Kwa mfano mtafitiwa mmoja aliposoma ujumbe “Unapepea na hujapimwa!”, ulimchochea kuchukua hatua inayofaa ya kwenda kupimwa ugonjwa wa ukimwi. Watafitiwa walitoa rai kwamba jumbe hizi huburudisha, huonya na hutoa mwelekeo mwafaka wa maisha kwa vijana wenzao mjini Nyahururu.

#### **4.4 Maoni ya wanaume.**

Watafitiwa katika kundi hili walikuwa wanaume ambao walikuwa na umri wa miaka kati ya ishirini na mmoja hadi miaka thalathini (21-30). Waliotafitiwa walikuwa hawajaoa kwa hivyo maoni yao kuhusu mada na umuhimu wa jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu yalikuwa tofafauti na maoni ya wale ambao walikuwa wameoa.

Mtafiti aligundua kwamba watafitiwa katika kikundi hiki huvisoma vibandiko vya jumbe katika magari ya matatu ambayo kwao ni nyenzo kuu ya usafiri wa kila siku. Waliotafitiwa walikuwa na elimu ya sekondari hadi chuo kikuu na walikuwa watu ambao wameajiriwa au hufanya biashara zao wenyewe.

Kundi hili la watafitiwa lilikuwa na baadhi ya wale ambao wanazipenda jumbe zilizowasilishwa katika mtindo wa Sheng. Wengi walishabikia jumbe katika lugha za Kiswahili na vile vile Kingereza, ingawa wengi walisema Kiswahili ni lugha ngumu kwao kwa sababu hawajaioea katika shughuli zao za kila siku hapa mjini Nyahururu.

Watafitiwa hawa walizipendelea jumbe zinazosheheni sajili za dini na siasa. Baadhi yao (asilimia arobaini) vile vile walipenda jumbe zinazozungumzia mambo ya ndoa na mahusiano ya wake na waume. Mtafiti alipotaka waeleze umuhimu wa jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu, maoni yalikuwa tofauti. Kuna wale ambao walisema kwamba jumbe hizi zinachochea hisia zao baada ya kuzisoma na kuzitafakari. Wengine walisema kwamba baada ya kuzisoma jumbe katika magari ya matatu wao huziwazia na zinawapelekea kurekebisha baadhi ya tabia ambazo jumbe hizi zinakashifu.

Kwa wale ambao walikuwa wakifanya shughuli za biashara, walidai kwamba jumbe zinazohimiza bidii na kutokata tamaa katika shughuli za biashara au wanapokosa kufanikiwa ziliwapendeza. Ujumbe uliotolewa na mmoja katika kundi hili na ambao unahimiza kuendelea kutia bidii ni huu:- “Jikaze ndugu shida haikupandwa kwako”. Wengine walisema kwamba jumbe hizi huwaburudisha na kuchekesha hasa baada ya kazi za kutwa nzima ambapo zinawasaidia kupunguza mawazo na kukabiliana na changamoto za kila kisu.

Mtafiti aliwahoji watafitiwa wengine ambao walikuwa na umri wa kati ya miaka thelathini na mmoja hadi miaka hamsini na zaidi (31-50 kuendelea). Miongoni mwa watafitiwa waliochunguzwa, wengi walikuwa wameoa na maoni yao kuhusu jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu yalikuwa tofauti kwa namna fulani na maoni ya wale ambao hawakuwa katika ndoa.

Lugha ya ujumbe iliyopendwa na watafitiwa katika kitengo hiki ilikuwa Kiswahili. Wengi walisema kuwa wanazielewa jumbe zilizowasilishwa katika lugha ya Kiswahili kuliko jumbe katika lugha za Kiingereza na Sheng.

Mtafiti alipata maoni mbalimbali kuhusu mada zinazopendwa zaidi na watafitiwa katika kundi hili. Mada kuhusu maisha kwa ujumla zilichukua nafasi kubwa katika kundi hili. Kwa kuelezea zaidi, baadhi ya watafitiwa walisema kwamba mada zinazohimiza watu jinsi ya kuwa na mahusiano katika jamii, haja ya kusaidiana na jumbe kuhusu kutii sheria za nchi ni baadhi ya mambo muhimu waliyoyazingatia.

Sehemu kubwa ya watafitiwa katika kundi hili (asilimia sabini) ilionyesha kupendezwa na jumbe kuhusu ndoa na mahusiano kati ya mume, mke, wazazi na watoto wao. Jumbe kuhusu siasa na biashara pia zilibainika kuchukuliwa kwa dhati na watafitiwa katika kundi hili.

Mtafiti alipowataka kutaja ni jumbe katika sajili gani ambazo walizipenda zipatikane kwa wingi katika magari ya matatu, ujumbe katika sajili ya dini ulipendwa zaidi kwa vile walihoji kwamba kizazi cha sasa hasa vijana kinahitaji nasaha kutokana na mafundisho ya kidini.

#### 4.5 Maoni ya wanawake.

Kundi hili la watafitiwa lilijumuisha wanawake wa umri kati ya miaka thelathini hadi hamsini (30-50). Mtafiti alibaini kwamba watafitiwa hawa walikuwa wakizisoma jumbe kwenye magari ya matatu katika mji wa Nyahururu.

Baadhi ya watafitiwa katika kikundi hiki walipenda jumbe zilizoandikwa kwa lugha ya Kikikuyu. Walieleza ya kwamba Kikikuyu ilikuwa lugha yao ya kwanza na walikuwa na umilisi mkubwa katika lugha hii. Hata hivyo, katika utafiti wake mchunguzi hakupata vibandiko vyo vyote katika lugha ya Kikikuyu isipokuwa vichache ambavyo vilichanganya Kiswahili na Kikikuyu.

Watafitiwa wengine walionekana walizipenda jumbe zilizowasilishwa kwa lugha ya Kiswahili na wengine walizipenda jumbe zilizowasilishwa kwa lugha ya kiingereza. Hali hii walisema ni kutokana na mfumo wa elimu walioupitia ambao ulisisitiza matumizi ya lugha hizi mbili. Aidha, walidai kwamba lugha hizi mbili za Kiswahili na Kingereza zilikuwa zimezoeleka kwao na kwa hiyo, hawakuwa na shida yo yote kuzielewa jumbe zilizoandikwa kwa lugha hizi.

Mtafiti aliwauliza watafitiwa kuhusu mada au sajili za jumbe ambazo walizichangamkia zaidi. Kwa kujibu, baadhi ya watafitiwa walizipenda jumbe zilizowasilishwa katika sajili ya dini. Walisema dini ni nyenzo inayotumika kuwafunzia na kuwapa hekima vijana. Wengine walidai kwamba ujumbe wa dini uliwapatia matumaini katika maisha na vile vile katika shughuli zao za kila siku.



Jumbe kuhusu maisha kwa ujumla pia ziliwavutia baadhi ya watafitiwa. Mada zilizopendwa katika jumbe hizi zilikuwa ndoa, maadili, uhusiano wa matabaka mbalimbali katika jamii kwa mfano matajiri na masikini, maswala ya utawala na mengineyo.

Kuhusu umuhimu wa jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu, waliotafitiwa walitoa rai kwamba jumbe hizi ziliwafahamisha kuhusu matukio tofauti kutoka sehemu mbalimbali za nchi, kuelimisha na kuadabisha, kuchekecha na kurekebisha mienendo na tabia zao.

#### **4.6 Maoni ya waandishi wa jumbe.**

Sehemu hii ya mwisho inachanganua maoni ya waaandishi wa jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu. Mtafiti alipowahoji baadhi ya waandishi wa jumbe hizi, ilibainika ya kwamba maandishi mengi yaliyoandikwa katika lugha ya Sheng yalipata wanunuzi wengi ambao wanamiliki magari ya matatu mijini na mashambani nchini kote.

Waandishi walipohojiwa walieleza ya kwamba wanawalenga wasomaji kutoka matabaka mbalimbali katika jamii, hivyo, lugha za Kiswahili na Kingereza zinatumiwa sana wakati wa kuandika jumbe kwenye magari ya matatu. Hii ni kwa sababu lugha hizi mbili zinatumiwa kwa wingi mjini Nyahururu na katika miji mingine nchini Kenya. Mtafiti aliwataka waandishi kubaini kusudi lao la kuandika jumbe zitundikwazo katika magari ya matatu. Kwa kujibu, waandishi waliotafitiwa walihoji kwamba wao walikuwa ni wafanyi biashara. Ni kupitia biashara hii ya kuandika vibandiko ambapo hulenga kupitisha jumbe muhimu kwa wasafiri kuhusu mada mbalimbali. Aidha, magari yaliyokuwa na vibandiko vya jumbe za kuvutia yalisemekana kuwa wavutia wasafiri wengi kuliko magari yasiyopambwa kwa jumbe hizi.

Kuhusu jumbe zinazopitishwa katika vibandiko vya magari ya matatu mjini Nyahururu, mtafiti hakupata ushahidi wa upotoshaji au kufasiriwa vibaya kwa jumbe hizi. Mtafiti alipowapa

baadhi ya sampuli za jumbe zilizofanyiwa utafiti. Maana yaliyokusudiwa ilifasiriwa vizuri na wasomaji waliofanyiwa utafiti kama ilivyoelezewa katika sura ya pili.

#### **4.7 Hitimisho.**

Tumeyachambua maoni ya wasafiri wanaoayaabiri magari ya matatu kuhusu jumbe za vibandiko mjini Nyahururu na vilevile waandishi wa jumbe zenyewe. Kwa ujumla, jumbe zilizoandikwa katika lugha tofauti tofauti ziliwavutia wasafiri na pia hisia kuhusu mada zilizozungumziwa katika jumbe hizi zilijitokeza kwa namna tofauti. Hata hivyo, maoni ya waliotafitiwa yalikuwa ni kwamba vibandiko hivi hubeba jumbe muhimu ambazo zinawaelimisha wasafiri kwa njia mbalimbali.

Katika sura ifuatayo na ambayo ndiyo ya mwisho, tumetoa tathmini ya muhutasari wa utafiti wetu pamoja na mahitimisho na mapendekezo kuhusu yafaayo kufanywa kuhusiana na mada kuu ya grafiti.

## SURA YA TANO

### MUHUTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Utangulizi.

Sura hii ambayo ni ya mwisho katika utafiti huu imeniua kujadili kwa kifupi matokeo ya utafiti wetu. Tumekusudia kubaini mchango wetu katika uwanja wa ki-akademia na pia kuzitathimini nadharia tete tulizoziorodhesha ili kutambua kama zinaunga mkono au zinapinga matokeo ya utafiti wetu. Mwishowe, tutatoa mapendekezo kwa watafiti wengine kuhusiana na mada yetu ya utafiti.

#### 5.2 Muhutajari wa matokeo.

Kutokana na utafiti wetu, tumegundua kwamba jumbe katika vibandiko vya magari ya matatu mjini Nyahururu zimeandikwa kwa mtindo wa grafiti. Mtindo huu umetumika sana katika takribani jumbe zote zilizochunguzwa. Mtindo huu ni maarufu kwa vile maandishi yake ni ya kuvutia kutokana na rangi tofauti tofauti zilizotumiwa. Vile vile, mtindo huu huziandika herufi kwa njia isiyokuwa ya kawaida na hivyo kuwafanya wasafiri kuziangazia kwa kuzisoma jumbe zenyewe kusudi wapate yaliyomo.

Uchunguzi wetu umeyatambua maandishi mengi katika lugha ya Sheng. Kama tulivyosema hapo awali, mtindo huu umesambaa sana kimatumizi mijini na mashambani nchini Kenya. Hali hii ilibainika katika mji wa Nyahururu ambapo Sheng ni lugha ya shughuli za kila siku miongoni mwa wakazi wa mji wa Nyahururu.

Sajili mbalimbali zimetumika katika jumbe tulizozishughulikia. Tumepata kuwa kuna matumizi mengi katika matumizi ya sajili ya biashara na vile vile sajili ya dini. Hata hivyo, ni jumbe chache kati ya zile zilizochunguzwa zilizotumia sajili ya magazeti.

Utafiti huu vile vile, umegundua ukiushi katika viwango vya kifonolojia. Utafiti umeonyesha uongezaji wa konsontanti /n/ na /d/ katika baadhi ya jumbe zilizotafitiwa. Ukiushi katika kiwango cha kisintaksia uligunduliwa hasa katika matumizi ya 'ni' na 'kwa'.

Utafiti wetu vile vile, umebaini matumizi mengi ya tamathali. Matokeo yameonyesha matumizi ya methali, sitiari, tasfida, chuku, kinaya na taswira katika jumbe tulizozishughulikia.

Watunzi wa jumbe zilizopatikana katika uchunguzi wetu walitumia mchanganyiko wa sentensi tofauti. Uchunguzi huu umegundua kuwa kuna jumbe zilizoandikwa kwa kutumia sentensi sahili kwa wingi. Tumepata jumbe katika sentensi ambatano na sentensi changamano ingawa si kwa wingi kama ilivyokuwa katika sentensi sahili.

Uchunguzi wetu umegundua pia kuwa jumbe ziliandikwa katika kauli mbalimbali. Tumegundua jumbe katika kauli yakinishi, kauli kanushi, kauli ya kushauri, kuonya, kuamrisha na kuomba.



### **5.2.1 Maoni ya wasafiri.**

Kuhusu maoni ya wasafiri wanaoyatumia magari ya matatu mjini Nyahururu, utafiti huu umeonyesha ya kwamba wasafiri walikuwa wakizisoma jumbe hizi katika magari ya matatu mjini Nyahururu.

Jumbe ambazo ziliwasilishwa kwa lugha za Kiswahili, Kingereza na Sheng zilikuwa na wasomaji wengi. Wasafiri waliotafitiwa na ambao walikuwa na umri wa kati ya miaka thalathini na mmoja hadi hamsini na kuendelea walionyesha kupendezwa na jumbe zilizowasilishwa katika lugha za Kiswahili na Kiingereza.

Watafitiwa ambao walikuwa na umri wa kati ya miaka kumi na mitano hadi ishirini walikuwa wanafunzi wa shule za sekondari. Utafiti umeonyesha kuwa jumbe katika lugha ya Sheng zilipendwa zaidi na watafitiwa katika kundi hili.

Kuhusu sajili, utafiti umeonyesha kwamba watafitiwa walikuwa na maoni tofauti. Hata hivyo, kiasi kikubwa cha watafitiwa walizipenda jumbe kuhusu maisha kwa ujumla, ilhali wengine walizipenda jumbe katika sajili za biashara na dini.

Utafiti wetu pia umegundua kwamba jumbe hizi zinatoa mchango mkubwa kwa wasafiri katika magari ya matatu mjini Nyahururu. Maoni ya watafitiwa yanaonyesha kwamba jumbe hizi ziliwafaa kwa kutoa nasaha, kuonya au kutoa tahadhari, kurekebisha tabia na kuadabisha. Aidha, jumbe hizi hufahamisha, huzindua, hupumbaza, hufurahisha, huchekesha na huburudisha wasafiri.

### **5.2.2 Kuhusu nadharia tete.**

Nadharia tete zetu tulizoziandaa zilikuwa nne. Tulichukulia kwamba jumbe katika magari ya matatu zinapuuzwa na wasafiri. Uchunguzi umebainisha kwamba wasafiri walikuwa wakizisoma jumbe hizi na kwa hivyo matokeo ya utafiti wetu yameipinga haipotesia hii.

Haipotesia yetu ya pili ilichukulia kwamba jumbe katika magari ya matatu zimelengwa hadhira anuai. Tumegundua kwamba jumbe zilizochunguzwa zililenga hadhira tofauti tofauti katika jamii na hivyo kuthibitisha haipotesia yetu.

Uchunguzi wetu pia ulithibitisha ya kwamba mitindo mbalimbali imetumiwa kuwasilisha jumbe katika magari ya matatu mjini Nyahururu, matokeo ambayo yanakubaliana na haipotesia yetu ya tatu.

Haipotesia yetu ya nne ilichukulia kwamba wasafiri katika magari ya matatu mjini Nyahururu walikuwa na maoni tofauti kuhusu jumbe zilizochunguzwa. Utafiti huu umebainisha dai hili kwa kuweza kupata maoni mbalimbali kutoka kwa wanafunzi, wafanya biashara na wakazi wengine katika mji wa Nyahururu.

### **5.2.3 Mapendekezo ya utafiti wa baadaye.**

Utafiti huu umeshughulikia mitindo katika jumbe kwenye magari ya matatu mjini Nyahururu. Ni muhimu swala hili la mitindo katika vibandiko vya magari ya matatu lishughulikiwe zaidi katika miji mingine midogo au mikubwa zaidi kuliko mji wa Nyahururu ili kubaini kama kuna tofauti zo zote kimtindo.

Hali kadhalika, utafiti huu wa kimtindo unaweza kugotanishwa na mitindo mingine kama vile grafiti katika mabweni na vyoo katika asasi zingine za elimu katika miji yetu ili kutathmini msambao wa mitindo mbalimbali katika uwasilishaji huu.

Watafiti katika mada hii yafaa wajiandae vilivyo kwa sababu utafiti wa aina hii una gharama kubwa za usafiri na wakati mwingine mtafiti ahitajika kuzipiga picha baadhi ya jumbe hizi ili zijitokeze katika uasilia wake.

## MAREJELEO.

- Crystal, D na Derek, D (1969) *Investigating English Style*; Longman Group.
- Daily Nation* (4<sup>th</sup> December, 2010). Page 5.
- Jeanire, A (2006) *The History of Graffiti*; London Global University
- Kazungu, E kadenge (1982) “*Deviation and Foregrounding in Chosen Swahili Literary Texts*”  
M.A. Thesis. University of Nairobi. (Haijachapishwa)
- Kingei, K.G. (1992) “*Advanced Language Skills in Kiswahili*” Lecture Series University of  
Nairobi.
- Kinyatti, M.L (2002) “ Language as a tool of Abuse Against Women”. The case of the  
Language of Matatu Touts and Male University Students in Nairobi. M.A Thesis; University  
of Nairobi (unpublished).*
- Leech, G (1983) *Principles of Pragmatics*; Longman.
- Levinson, S.C (1983) *Pragmatics*: Cambridge University Press.
- Masokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*; East African Education Publishers.  
Nairobi.
- Mathooko, M (2007) *Isimu Jamii; Misingi na Nadharia*; Njugu Books Nairobi.
- Mbatiah, M. (2000) *Kamusi ya Fasihi*; Standard Textbooks, Graphics and Publishing. Nairobi.
- Mweri, G. (2010) *Utangulizi wa Isimu*; Kenya Literature Bureau, Nairobi.
- Ndungo, C.M na Wafula, R.M (1993) “*Nadharia ya Fasihi*”. Makala ya kufundishia Chuo  
Kikuu Cha Nairobi.
- Njogu K, na Chimerah, R (1999) *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia wa mbinu*; Jomo Kenyatta  
Foundation – Nairobi.



- Nyauncho, Osinde Ken (1986) *Sheng: an Investigation into Social and Structural Aspects of an evolving Language*. Dissertation (B.A.) University of Nairobi. (unpublished)
- Nwoye, O. (1993). *Social Issues on Walls; Graffiti in University Lavatories, Discourse and Society*. Vol. 4 (4), 419 – 442.
- Onchiri, H (2010) “*Graffiti Perspective on Matatus in Kenya*”. M.A Thesis ; University of Nairobi. (Haijachapishwa)
- Shake, R (1991) “ *Ukiushi Katika Lugha ya Kimaongezi Dhidi ya Kanuni za Kiswahili Sanifu*”. M.A Thesis; University of Nairobi. (Haijachapishwa).
- TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*; Oxford University Press. Dar es Salaam
- Wamitila, K.W (2003) *Kamusi ya Fasihi; Istihali na Nadharia*: Focus Publications Ltd. Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (2004) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*: Focus Brooks, Nairobi.
- Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Oxford University Press, London.


## Kiambatanisho (i)

Hii ni orodha ya jumbe zilizopatikana kwenye magari ya matatu mjini Nyahururu. Idadi ya vibandiko ilikuwa kubwa lakini baadhi ya jumbe hizi zilikuwa zimerudiwarudiwa katika magari ya matatu mjini Nyahururu. Baadhi ya jumbe zilizoorodheshwa hapa hazikuchanganuliwa kwa vile havikuchangia katika mada yetu.

1. Lipa nauli bila shinda.
2. Ridhika kwa kile umepata
3. Karau alipe gari!!!
4. Chuki nichukie lakini roho yangu niachie
5. Dere yuko poa
6. Hatutakaa saana
7. Wewe ni wetu (rangi tofauti)
8. Kazi ni Kazi bora mtu asukume maisha
9. Ubaya wa Marehemu hakutumia juala
10. Uliza ujibiwe uliza ujinga utusiwe
11. Usiharakishe driver, wewe ndiwe umechelewa.
12. Usiniulize kuhusu maisha yangu, subiri hadi nife Historia yangu itasomwa.
13. Jikaze ndugu shida haikupandwa kwako.
14. Utajipangaje kama haujijui?
15. Mwenye wivu ameze wembe.
- 16.. Kunyemelea mke wa mwingine ni kama ng'ombe kujipeleka kichijio.
17. Chunga mzigo wako!
18. Ulinisaidia wakati wa shida ikawa siri yetu sasa unanitangaza kwa wenzako
19. Usiteme mate hapa, si una handbag?
20. Hatusemi wewe ni mnono, lakini ukikalia viti mbili, LIPIA.
21. Unapepea.. na VCT hujaenda.
22. Kupanda ni popote kushuka ni stage.
23. Ili nifanikiwe nahitaji marafiki, ili nifanikiwe zaidi nahitaji maadui.
24. Kama una haraka shuka ukimbie.
25. Wivu wako ndiyo bahati yangu.
26. Kaa nao ujue tabia zao.
27. Conductor ni wa maana sana hutubebea watu bila ukabila.
28. Hata nikipimwa hakuna dawa.
29. Unaringa, je umepimwa?
30. "Juzi ilikuwa sare, jana vilevile, sasa leo lipa cash."
31. Heri kununua gari kuliko kuoa mke mkorofi.
32. Lipa deni la wenyewe na utabarikiwa.
33. Lipa bila fujo.
34. Yenu moyoni, ya wenzangu mdomoni.

35. Naishi niwezavyo siishi mtakavyo.
36. Usiniite mjinga kwa kuniona mpole.
37. Dunia sio mbaya watu ndio wabaya.
38. Mganga wangu ni Yesu, jaribu wako mashuhuri.
39. Safari ni ndefu lakini nikiwa na Yesu nitashinda.
40. Mheshimu mjinga uepukane na balaa.
41. Biashara yangu haitaki mchezo.
42. Unajifanya redio kutangaza ya wenzako na yako yamekushinda.
43. Ukinicheka leo, kesho watakucheka
44. Ukiwa kwa gari unajifanya mkali na ukifika kwa nyumba wewe ni bubu.
45. Ombea adui yako aishi siku nyingi ili unapobarikiwa ashuhudie mwenyewe.
46. Usitoe viatu kwa gari
47. Usinione nimetupa mbao haja ndizo nyingi.
48. Anayekamua ng'ombe wa jirani arambe moto
49. Yule manzi ametuvalia chupa leo.
50. Utamaliza pesa zako kwa waganga na utaniacha vile vile.
51. Pilipili usiyoilala yakuashia nini?
52. Utamu wa kazi ni pesa.
53. Usiidharau kazi yangu, yako hainisaidii.
54. Ata ukipimwa sitaki.
55. Hii kazi ni ngumu, tafadhali lipa bila fujo.
56. Ukiingia kwa mat, usitoe viatu lakini toa fare.
57. Fanya fujo uone!
58. Mkopo ni adui wa biashara.
59. Mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe; bila jasho hupati.
60. Unatengeneza kwa wengine kwako kwaporomoka.
61. Kazi kwa vijana, pesa kwa wazee.
62. Wewe ni kiherehere sana, lakini ukifika kwangu fungua mdomo.
63. Ukifuata ukabila utakaa bila.
64. Nitaishi naye kwa raha na taabu.
65. Nakupenda lakini biashara yangu haikutambui.
66. Watasema mchana usiku watalala.
67. Wacha ugicagi!
68. Msiegemeane kwa gari kama hamujuani.
69. Tafadhali jifunge mshipi.
70. Umejifunga mshipi?
71. Usinione unidharau, naweza kuwa usaidizi wako.
72. Asiyejua kulipa aogope kukopa.
73. Jiepushe na madeni, usidaiwe hadharani.
74. Hakuna stage ya (kumi)
75. Neema ya Bwana Yesu Kristo iwe pamoja nanyi (green).
76. G jua hali yako ya HIV.

**Kiambatanisho (ii)**



Lawani Ya Mj. Wa Nyakuumu

- Priority 1
- Priority 2
- Priority 3
- Mainly Bus Routes